

ROHO WA KWELI



... amini.

Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu sasa wakati tukiomba. Na tuinamishe vichwa vyetu.

² Baba yetu mwenye haki wa Mbinguni, tunapokukaribia Wewe sasa katika Jina hilo litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, tunataka kukupa Wewe sifa kwa ajili ya yale Wewe umetufanyia, yale macho yetu yameona, na masikio yetu kusikia katika siku hizi za mwisho za mandhari ya kuimalizia historia ya ulimwengu huu, huku wakati ukififia ukaingia katika Umilele, nasi tunaona Nuru zikiangaza, tunajua si muda mrefu sasa hata Kuja kwa Bwana Yesu.

³ Tungekuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, utukumbuke usiku wa leo. Na iwapo kuna uovu wowote ndani yetu, uondoe, Bwana, usiku wa leo, tupate kuwa wanaopendeza Kwako kama ungekuja usiku wa leo. Tunawaombea wagonjwa na wahitaji.

⁴ Tunaliombea Kanisa Lako, hapa na ng'ambo pia, kote ulimwenguni, wototo Wako kila mahali wa kila taifa, tupate kuosha mavazi yetu katika Damu ya Mwana-kondoo, na tukilisikiliza wito huo, "Tazama, Bwana-arusi yuaja. Haya tokeni mwende mkamlaki." Jalia tuweze kwenye wakati huo, Bwana, kwa neema ya Mungu, na kwa ustahilifu wa Yesu Ambaye tunamtumaini, tupate kuzisafisha taa zetu na tusonge mbele basi kumlaki Bwana-arusi. Litwae Neno la Bwana usiku wa leo na uitahiri mioyo yetu. Ondoa kutokuamini kwote. Tupe ibada kuu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵ Hakika ni vema kurudi hapa katika... madhabahu haya ya Bwana, usiku wa leo, katika ibada. Tulikuwa na wakati mzuri sana jioni huko kwa... Ndugu Groomer. Nami ninakumbuka mwaka jana tulikuwa na wakati mzuri mno.

⁶ Tumekuwa na wakati wa ajabu, kila mahali. Bwana ndio kwanza atubariki mno, kuliko vile nilivyopata kuwazia Yeye angefanya. Lakini Yeye amejaa sana rehema na wema. Ni vizuri tu kumjua. Sivyo? Na kuwazia, "Kumjua Yeye, ni Uzima." Kumjua Yeye, ni Uzima.

⁷ Sasa, kesho usiku, tutakuwa huko chini katika Central Avenue Assembly, ninaamini ndivyo linavyoitwa. Ndugu Fuller, ndugu mwingine mzuri. Nami nafikiri ni kanisa kubwa kule chini. Nasi tunatumaini kwamba labda tunaweza kuwa na m—mstari wa maombi, ikiwa ni sawa na Ndugu Fuller. Kwa hiyo sisi...

⁸ Halafu basi, ke—kesho yake asubuhi, tutakuwa kwenye, ninaamini, linaitwa Kanisa la Kimitume hapa Phoenix. Na sikumbuki tu kwamba mchungaji wake ni nani, ndugu yule, aliyekuwa. Nilikuwa kule mwaka jana? [Ndugu fulani anasema, “La. Hilo ni jipya, kanisa la Kimeksiko, Ndugu Branham.”—Mh.]

⁹ Halafu Jumapili usiku kwenye kanisa la Ndugu yetu wa thamani Outlaw huku juu, Kanisa la Jesus’ Name. Nami nina matarajio makubwa, na familia yangu, kuingia kule na kusikia baadhi ya huo uimbaji mzuri.

¹⁰ Billy Paul anapaswa kuujua, kila mmoja, kwa moyo. Tuliucheza wimbo huo, *Ninapaa Juu, Juu*, mpaka, kusema kweli, kitu hicho kimechakaa, kwenye kanda. Ataanzia ofisini, na kila wakati wa mchana ninapoenda kule, haidhuru, yeye anaucheza huo, “Juu, juu, juu.” Ni kitu fulani! Tumeucheza kupita kiasi, na hiyo santuri karibu imechakaa kabisa.

¹¹ Mwajua, kidogo nilikuwa na hisi usiku wa leo, kwamba, kidogo nimepwelewa na sauti, nikawaza, “Jamani, laiti ningalimwona mtu fulani, angaliweza kuhubiri kwa niaba yangu,” basi ikawa niliangalia huku na kumwona Jack Moore. Ni kweli tu kabisa. Kamwe sikuninii. . . Loo, ninaamini hilo lingekuwa tu ni zuri sana, Ndugu Jack. [Ndugu Jack Moore anatoa mawazo—Mh.] Sasa lisikilizeni hilo.

¹² Nami ninaamini ninamwona Ndugu Roy Borders ameketi hapa nje, pia. Naam, bwana. Ndugu Noel Jones ameketi huku. Loo, jamani! Tuko kote, kila mahali. Nafikiri ungekuwa ni wakati mzuri, labda, kama ningepumzika kidogo, mwajua, na niwe na baadhi ya watu hawa wazuri wakija hapa na kuhubiri kwa niaba yangu ninapopwelewa na sauti, mwajua. Ndugu Jack alisema, “Bwana hayuko katika ufunuo huo.” Vema, nilikuwa mchovu nilipokuja. Nami—nami nimekuwa mchovu kidogo, wakati wote.

¹³ Nami ninawaona watu wamesimama pale, na jinsi inavyowabidi kusimama, na kwa namna fulani ninafurahi kwamba ninasimama pamoja nao. Sasa, Bwana awabariki.

¹⁴ Nasi sasa tunaitazamia mikutano hii mingine inayokuja. Halafu juma lijalo ni huko kwenye Pentecostal Assemblies, na huko juu. Nasi tutamalizia, Jumatano ijayo usiku, kwenye ya 11 na Garfield. Siwezi kuikumbuka yote akilini. Kwenye, ninaamini, First Assembly of God mjini. Halafu—halafu basi ule mkutano utaanza huko Ramada.

¹⁵ Na sasa kuna dhifa kwa ajili ya Wafanyabiashara chini kwenye m—mji mkuu wa Arizona: Tucson.

¹⁶ Na hakika, sote tunajua ya kwamba Phoenix na sehemu hizi, vitongoji tu vya mji huo. Na hiyo ni kweli. Hapo ndipo mahali muhimu. Huo ndio mji wangu wa nyumbani, mwajua, kwa hiyo, na kwa hiyo, huko juu mlimani. Na halafu huu, ninii tu, namna

ya vitongoji vyake, mbona, ni vema kuwa nanyi nyote kama majirani, kwa hiyo. . .

¹⁷ Naamini ilikuwa ni Ndugu Rasmusson, usiku mmoja, aliyesema jambo kama hilo mkutanoni, ndipo, loo, jamani, karibu auvuruge mkutano wote. Ninaamini tulikuwa kwenye—tulikuwa Houston. Na ilikuwa ni Ramsar. Ilikuwa ni huyo. Yeye alisema, ule usiku Malaika wa Bwana aliposhuka, wakapiga picha, ndipo akasema, “Ninyi watu wote mlio karibu hapa kutoka—kutoka Dallas,” kasema, “tunajua hivyo ni vitongoji vya Houston.” Ndipo, loo, jamani! Texas isingelivumilia hilo, kadiri ya vile ninyi Waarizona mngeliweza. Kwa hiyo kulikuwa na unyamavu mkubwa mkutanoni.

¹⁸ Vema, Yeye ni mwema sana. Na sasa nafikiri tutayafungua Maandiko hapa, na kutoa tu ushuhuda kidogo kwa muda mfupi. Hilo si lingelibadilisha kidogo? Nimelitwanga tu kwa nguvu sana hata ninaona aibu kuwaangalieni. Na labda niwape raha kidogo, na kutoa ushuhuda wa fadhili za Bwana.

¹⁹ Hebu tupate mahali katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 16 wa Yohana Mtakatifu. Nami nina 16:12. Ningetaka kusoma kutoka—kutoka mahali hapo katika Injili ya Yohana Mtakatifu. Ninapenda kulisoma Neno, kwa sababu Neno ndilo linalotufanya kujua kwamba ni Kweli. Kuanzia kwenye kifungu cha 12, basi sikilizeni kwa makini sasa, maana ninataka kutoa ushuhuda.

²⁰ Na kisha tutajaribu kuingia mapema kidogo tu. Nimekuwa nikiwachelewesha sana. Halafu kesho usiku, mbona, tutakaa nusu saa zaidi. Hiyo itaifanya karibu saa saba, sivyo?

Kwa hiyo, kwa hiyo, hii ni kuanzia kwenye kifungu cha 12:

Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa.

Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawaonyesha.

Yeye sasa atanitukuza mimi: kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.

Yote... aliyo nayo Baba ni yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo yangu, na kuwaonyesha.

²¹ Mnajua, jana jioni, hasa, tulikuwa na sampuli ndogo ya hilo. Sasa, sisi tukiwa ni watu wa Full Gospel, tunaamini katika kazi zote za Roho Mtakatifu. Na sasa, hivyo ndivyo tu tunavyoweza kuwa Full Gospel, ni kuamini Injili yote, yote aliyoandika Bwana. Nami ninaamini kwamba sisi, wenyewe, si kitu. Sisi ni kama tu. . .

²² Kama nilivyomwambia Ndugu Carl, jana, nikiuangalia mti fulani, nilisema, “Huo si ni mti mzuri wa mtende? Lakini, hata hivyo, huo si kitu ila lundo la majivu ya volkano. Hivyo tu ndivyo ulivyo.” Kisha nikasema, “Jinsi ulivyo tofauti sasa na ule mkalitusi. Vema, mti wa mkalitusi ni nini? Majivu ya volkano, yaliyo na uhai ndani yake.” Kisha nikasema, “Hata hivyo, mimi ni nini na wewe ni nini? Majivu ya volkano, hiyo ni kweli kabisa, kutoka ardhini; mavumbi ya ardhini, yenye uhai ndani yake.”

²³ Lakini kila uhai umepandwa na mpaji mkuu wa Uhai, na Yeye anajua tu namna na kile cha kufanya. Na kila kitu ambacho Yeye ameweka hapa duniani ni kwa ajili ya utukufu Wake. Nyota ni kwa ajili ya utukufu Wake. Upepo ni kwa ajili ya utukufu Wake. Maua ni kwa ajili ya utukufu Wake. Na sisi ndio ukamilifu wa utukufu Wake.

²⁴ Lakini inaonekana kana kwamba kila kitu kitamtii Yeye ila mwanadamu. Mwanadamu anaonekana tu kuninii. . . Yeye ana wakati mgumu sana, kwa sababu kwamba ndiye kitu cha pekee kilichoanguka. Kila kitu kingine kilikaa mahali pake pa asili. Lakini, mwanadamu alianguka. Kwa hiyo, Mungu ana vita naye, kumfanya atende yaliyo haki, na kutii.

²⁵ Basi moja ya matatizo makuu ya Mungu, kote katika miaka, kama vile historia ya kanisa inavyoelezea, ni kumpata mtu ambaye Yeye anaweza kumweka chini ya mamlaka Yake kabisa. Yeye anahitaji tu mtu mmoja. Daima Yeye amemtumia mtu mmoja kwa wakati mmoja. Tulisoma hilo siku chache zilizopita usiku: mtu mmoja, sio kundi. Yeye anahitaji tu mmoja. Huyu tu ndiye anahitaji. Sababu, watu wawili wangukuwa na mawazo mawili tofauti. Yeye, basi, humfanya tu mtu mmoja, hujiwakilisha Mwenyewe kupitia mtu huyo mmoja. Kamwe hakufanya vinginevyo ila hivyo. Mnaona?

²⁶ Sasa, Yeye yuna Mtu mmoja leo hii, naye Mtu huyo Ndiye ambaye tumesoma tu habari zake: Roho Mtakatifu. Ndiye Mtu ambaye Mungu amemtuma, Roho wa Yesu Kristo duniani, Roho wa Mungu, kudhihirisha na kumtangaza Kristo kupitia Kanisa Lake, mnaona, kuendeleza tu Uhai wa Kristo kupitia Kanisa.

²⁷ Sasa, ni jambo la ajabu sana, na—na hata hivyo ni rahisi sana, iwapo tungetulia tu na kutafakari. Tunasukuma, tunatetemeka, tu—tunahofia, tunaingia katika vurugu na mashaka, kuwazia tu. “Vema, lazima nijitahidi kuingia. . .?” Si hivyo. Ni kujitolea tu, mnaona, kutambua ya kwamba wewe si kitu, na kumwacha Yeye akutawale kabisa, ayachukue mawazo yako, achukue mamlaka.

²⁸ Sasa, simaanishi kumwendea Kristo ukiwa—ukiwa tu na ni—nia iliyo tupu. Simaanishi hilo. Njoo Kwake ukiwa na akili timamu, na katika ni—ni—nia ya toba, na nyenyekevu. Ndipo useme, “Bwana Yesu, mimi hapa. Sasa, imeandikwa hapa katika Neno Lako, ya kwamba Wewe ‘ulikuwa na mambo mengi ya

kuwaambia wanafunzi.’ Ulisema, ‘Wasingeweza kuyastahimili hivi sasa.’” Na labda ndiyo hali yetu leo hii, hatuwezi kuyafahamu.

²⁹ Mungu anaweza kuinua kitu fulani kidogo tofauti, na kwa pamoja tunakikataa kabisa hadharani. Badala ya kuchunguza Maandiko kuona kama ni kweli ama si kweli, upesi tunakitupilia tu mbali, “Hakuna kitu kwake.” Inatupasa kuyachunguza mambo haya, tuone kama ni kweli ama si kweli. Pia kumbukeni, iwapo si kweli, yatakufa hatimaye, kwa kuwa Yesu alisema, “Kila mmea ambao Baba Yangu wa Mbinguni hakuupanda utang’olewa.”

³⁰ Lakini nafikiri ilikuwa ni Gamalieli ambaye alitoa tamshi lile kuu wakati ule, “Kama ikiwa ni ya Mungu, hatutaki kuonekana kuwa tunaipiga vita. Na—na kama si ya Mungu, itavunjika haidhuru.” Kwa hiyo, lichunguzeni na kulitafakari.

³¹ Na sasa, Yeye alisema hapa ndani, “Lakini Huyu, Roho Mtakatifu, atakapokuja.”

³² Sasa, mtu fulani alisema, imekuwa ni muda fulani uliopita, akinena, alisema, “Roho Mtakatifu kwa kweli ni nia yako ya kiakili. Unawaza.” Hilo lingemfanya Roho Mtakatifu kuwa ni wazo.

³³ Lakini Biblia ilisema, “Wakati Yeye...” Basi “Yeye” ni kiwakilishi nafsi. Mnaona? Mnaona? “Wakati Yeye,” Mtu, Roho Mtakatifu, Mungu, “atakapokuja, Yeye atawafunulia mambo haya, ambayo nimewaambia.”

³⁴ Halafu, mnaona, hakuna njia nyingine ya kujua Kweli ni nini. Ila tu kwa... Huwezi kuipata kwa utamaduni, kwa ujuzi wa seminari. Utaipata tu kwa Roho Mtakatifu. Yeye Ndiye aliyetumwa kuifunua.

Sasa, basi, pia Yeye alisema, “Na Yeye atawaonyesha mambo yajayo.”

³⁵ Sasa, Waebrania, mlango wa kwanza, ilisema, “Mungu zamani za kale na kwa njia mbalimbali alinena na baba zetu kupitia manabii, lakini katika siku hizi za mwisho kwa Mwanawe, Kristo Yesu.” Mnaona? Ni Roho Mtakatifu akimiliki, ama akichukua mamlaka juu ya Kanisa, kumfanya Kristo atende kazi Kanisani. Ndipo, wewe unakuwa kama Yeye alivyokuwa. Yeye anakuwa kama ulivyokuwa wewe, kusudi uweze kuwa kama alivyokuwa Yeye. Mnaona? Yeye anafanyika wewe, ili uweze kufanyika Yeye. Hiyo, i—inapita ufahamu. Hakuna njia ya kulielezea, wala usijaribu. Likubali tu. Yeye alilineni, na hilo latosha. Sema tu ni kweli, liamini.

³⁶ Sasa, kama Mkristo mchanga, sikuzote nimetoa tamshi hili. Nilifurahi Mungu alinishika kabla kanisa halijanishika. Ni vigumu kujua jinsi ningalikuwa. Lakini mimi—mimi nilishukuru kwa huo uongozi na mawasiliano ya moja kwa moja ambayo

Roho Mtakatifu alitia maishani mwangu, kabla sijajitolea kwake. Kwa kuwa, kama mtoto mdogo, nilijua kulikuwako na Kitu fulani. Yeye alikuwa amezungumza, nami ningezungumza na Yeye. Alinijibu. Ndipo nikaanza kuona ya kwamba mambo aliyoniambia, kama mtoto mdogo, ya kwamba yalianza kutukia jinsi hasa Yeye alivyosema yangetukia. Kwa hiyo nikajua kwamba ilibidi yawe ni kweli.

³⁷ Sasa, mimi ni mzee sasa. Na mimi—mimi kamwe hata wakati mmoja. . . Na ninaweza kuuita ulimwengu ku—kutulia kabisa, na kuwauliza. “Wekeni kidole chenu juu ya jambo moja ambalo Yeye aliwahi kuniambia, katika BWANA ASEMA HIVI, katika Jina la Bwana, ila lile lililokuwa kabisa ni kweli na hakika, nalo lilitimia, kutoka kwenye maelfu mara maelfu ya mambo.” Ni nini. . .

³⁸ Kwa nini ninasema hilo? Mnaona, nimeweka sisi sote kama mavumbi ya volkano. Lakini ni ahadi ya Neno la Mungu. Kwa hiyo, siwezi kuwa na imani na nafsi yangu. Huwezi kuwa na imani na nafsi yako. Lakini, kwa pamoja, tunaweza kuwa na imani na Kile ambacho kimechukua mamlaka juu yetu. Roho Mtakatifu amechukua mamlaka juu yetu. Hatuna budi kuwa na imani na Huyo. Na tunapoweka matumaini yetu katika Huyo, basi matokeo yanakuja.

³⁹ Ingekuwa hakuna sababu kwangu mimi kujaribu hata ku—kuwadokezea fununu ya baadhi ya mambo ambayo Roho Mtakatifu amefanya katika maisha yangu mwenyewe yaliyovunjika-vunjika, siku zangu. Ninasema hili huku Biblia Yake imefunguliwa, Neno Lake. Na hilo ndilo alilo Yeye. Yeye ni Neno.

⁴⁰ Mnaona, hii—hii Mbegu hapa inaingia kwenye mavumbi ya volkano, kwa njia ya Kiumbe cha kiroho. Mungu huingia kama Roho na anafanya kazi kupitia kwa mavumbi. Kwa hiyo, si mwanadamu. Ni Mungu.

⁴¹ Na kama ningeleti chini, na kuchukua wakati kuyaandika mambo ambayo nimemwona Yeye akiyafanya, ingechukua vitabu vingi. Basi kulitafakari, hapa, umri wa miaka hamsini na mitatu, na ninaweza kusema mbele za Mungu, Kanisa Lake, na Biblia, mbele ya kundi hili, kwamba, “Sijaona hata wakati mmoja Hilo likishindwa; huwa kamilifu juu ya alama, kila wakati.”

⁴² Isipokuwa, hivi majuzi wakati nilipokuja magharibi. Mmeicheza hiyo kanda, wengi wenu, nadhani, mnaelewa. Sijui nini. Ninangojea. Nipo hapa sasa. Sijui ni kwa nini. Ninangojea tu.

⁴³ Huenda ikawa ni wakati wangu wa kwenda nyumbani. Inaonekana zaidi sana hivyo. Kama ndivyo, atainuka mtu fulani baada yangu, ambaye atauendeleza Ujumbe. Atakuwa ni mtu wa

kipekee, bali atainuka baada ya haya na kuendeleza Ujumbe. Nanyi usikilizeni. Mradi tu ni Maandiko, dumuni nao.

⁴⁴ Kama sivyo, kunakuja sehemu nyingine sasa, kwa kuwa ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho, nami ninashukuru ya kwamba nimeishi katika siku hii. Nisingeibadilisha siku hii na siku yoyote. Hii ndiyo siku tukufu zaidi iliyowahi kuwako juu ya nchi. Hakuna siku nyingine ambayo imewahi kuishinda siku hii.

⁴⁵ Loo, vipi kama Musa, Eliya, Paulo, Sila, hao mashujaa mashuhuri wa imani, katika siku zilizopita, wangeweza kuinuka na kuchukua kitabu cha historia, na kuangalia hasa yale waliyokuwa wametabiri, yakitimia, na kuona mahali tulipo sasa? Mbona, wangewaweka gerezani, katika saa moja. Bila shaka. Wangekuwa kama watu wa mwituni, huku na huku mitaani, kwa nguvu tu kama walivyoweza, wakiitangaza Injili. “Wakati umewadia.” Ndipo tunaona, usiku wa leo, ya kwamba tunapungukiwa sana na utukufu wa Mungu.

⁴⁶ Lakini ningetaka kurudia tu mara moja, kidogo kulifanya kanisa. . .

⁴⁷ Jambo lingine, hivi Billy Paul alisambaza kadi za maombi katika kanisa hili usiku wa leo? Ndio kwanza nitoke Tucson dakika chache zilizopita. [Mtu fulani anasema, “Naam.”—Mh.] A—alilisambaza kadi. Sasa, hiyo itakuwa ni njia mbaya sana ya kujaribu kuwaleta. Tutajaribu.

⁴⁸ Sasa, sitachukua muda mrefu sana, kutoa tu ushuhuda juu ya Andiko hili.

⁴⁹ Ya kwamba, Kristo hutimiza Maneno Yake yote. Hana budi kuyatimiza. Hana budi kufanya jambo hilo. Mnaona? Hainibidi kuyatimiza; mimi ni mwanadamu, anayeweza kufanya makosa. Yeye ni asiyepatikana na mauti, asiyeweza kukosea. Hana budi kutimiza Yake. Mnaona? Bali hainibidi kutimiza yangu. Haikubidi kutimiza yako. Bali Yeye hutimiza. Loo, hivi hilo haliliweki jambo fulani ndani yako, kujua ya kwamba Yeye—Yeye anawajibika kabisa kwa Neno hilo?

⁵⁰ Na, kwamba, juma hili, jinsi ambavyo tumepitia kwenye Biblia, pamoja na hao manabii na wazee wetu, na kila wakati tukaonyesha ya kwamba wakati kanisa lilipoliondokea hilo, Mungu alituma mtu fulani na kuwatikisa wakarudi kwenye Neno hilo tena, kulinyosha kanisa. Imekuwa hivyo daima. Hiyo ndiyo sera ya Mungu. Yeye aliwachagua wanadamu kufanya hivyo.

⁵¹ Sasa, kama angekuwa amechagua nyota kuhubiri Injili, ingalitendeka muda mrefu uliopita. Kamwe zisingalienda nje ya mapenzi Yake. Kama angalilichagua ju—jua kuihubiri, ama u—upepo kuihubiri, kamwe usingeenda nje ya mapenzi Yake. Mnaona?

⁵² Lakini sisi tuko kwenye msingi wa hiari ya kujichagulia wenyewe. Tunaweza tukatenda jinsi tupendavyo. Na hiyo ndiyo sababu tumekuwa wasumbufu hivi Kwake. Sikuzote *hivi*, na kutaka kuingiza njia zetu wenyewe, na kuziondokea njia Zake. Mnaona?

⁵³ Na mimi—mimi nimesema hapo awali, mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale aliyofanya. Na daima anasema yale Yeye atakayofanya. Halafu basi, wakati uo huo, akiyapuuza yale anayofanya. Mnaona?

⁵⁴ Mwanadamu atasema, “Loo, Mungu alifungua Bahari ya Shamu. Naam. Utukufu kwa Mungu! Hiyo ni kweli.” “Naam, Yesu yuaja tena. Haleluya! Hiyo ni kweli.” Lakini, kuna kumhusu siku hizi? “Aa, hiyo ilikuwa kwa ajili ya siku nyingine.” Mnaona? Mnaona? Sikuzote ni yale aliyofanya, yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya.

⁵⁵ Hiyo ni hali zile zile ambazo Yesu alipata hapo alipokuja duniani. Kweli kabisa. Mungu alikuwa ameahidi yale aliyokuwa amefanya. Na alikuwa ndiye Huyu hapa, amesimama mbele zao, nao hawakumtambua. “Alikuwako ulimwenguni, na ulimwengu uliumbwa na Yeye, wala ulimwengu haukumtambua.” Hiyo ni kweli.

⁵⁶ “Bali wote waliompokea, hao aliwapa uwezo wa kuwa wana wa Mungu.” Hiyo ndiyo sehemu adhimu.

⁵⁷ Ilikuwa ni wakati fulani uliopita, maskini ono fulani ningetaka kuwazungumzia kulihusu. Na mimi sijui, huenda kamwe sijalisema ila kwa mtu mmoja tu mahali fulani. Lakini ndiyo kwanza ni—nimpoteze mmoja wa watu walio wakuu sana duniani, kwangu mimi, mama yangu.

⁵⁸ Na mimi—mimi ninampenda mama yangu. Jinsi ambavyo ningemwona akitoka mezani, wakati tulipokuwa maskini sana, hatukuwa na chochote cha kula! Naye. . . Papa angeleta mkate, ambapo angeuokota kutoka dukani, ama kitu fulani, na—nao wangeumwagia kahawa, kisha waweke sukari juu ya huo. Naye mama angejifanya kana kwamba hakuwa na njaa, kusudi sisi watoto tuweze kupata kitu cha kula. Loo, si—siwezi kamwe kusahau hilo. Mnaona? Na mara nyingi ambapo angenichukua, na mambo aliyonifanyia. Lakini, mwajua, Mungu ni—ni mwingi sana wa rehema. Yeye anaelewa mambo hayo yote, wakati inapombidi kuyachukua. Na mimi—mimi nampenda kwa ajili ya jambo hilo.

⁵⁹ Daima imekuwa, kwamba, kabla yeyote wa watu wangu kufa, ninaliona kabla halijatukia, katika ono.

⁶⁰ Nilimwona kaka yangu, nilipokuwa tu na umri wa miaka kumi na minane, kumi na tisa. Nilimwona kabla hajaondoka. Hata sikuwa Mkristo, bali niliona ono likija mbele zangu, nikamwona ndugu yangu akiaga dunia.

Nilimwona baba yangu wakati alipoondoka.

⁶¹ Howard, wengi wenu mnamkumbuka Howard. “Howard,” mnanikumbuka mimi, miaka miwili kabla halijatukia, nilisema, “Howard, nilipaona mahali pako pametiwa alama. Ndiwe utakayefuata.” Nikasema, “Jiweke sawa, ndugu, kwa sababu ndiwe utakayefuata kuondoka.” Naye akaondoka, vivyo hivyo hasa. Halafu basi, hapa wakati fulani uliopita . . .

⁶² Sasa, natumaini hili halitasikika la kukufuru, lakini, kuonyesha tu ku—kujali kwa Mungu. Mungu daima anajali katika mambo madogo, kama yale makubwa. Ninataka kusema jambo hili kwa manufaa ya baadhi ya wahubiri hawa wazuri. Kwamba labda . . . Nami ninajijumuisha humo ndani.

⁶³ Sasa, sisi, kila mmoja, tungetaka kuwa Billy Graham, bali sisi . . . Nasi kila mmoja tungetaka kuwa Oral Roberts. Lakini, sisi, sisi si Billy Graham wala Oral Roberts. Sisi ni watumishi wa Mungu kwenye huduma ambamo Yeye ametuweka. Mnaona? Haidhuru ni ndogo jinsi gani, ama ni kubwa jinsi gani, ni sawa tu machoni pa Mungu, daima ni sawa, kufanya kazi pale pale mahali ulipo. Daima, ni jambo zuri sana kumfuata Bwana.

⁶⁴ Afadhali nishinde . . . ama niende na kuwa na kanisa lenye watu hamsini ndani yake, katika mapenzi ya Mungu, kuliko kwenda kuwa na elfu tano nje ya mapenzi ya Mungu. Hakika. Mungu anaweza kufanya mengi zaidi pamoja na mtu aliye katika mapenzi Yake, katika saa moja, kuliko angaliweza na mtu aliye nje ya mapenzi Yake, katika miaka hamsini. Mnaona? Yeye anajikwaa na kupepesuka, kama kupiga risasi gizani. Lakini wakati mtu yuko kabisa katika mapenzi ya Mungu, na anajua wito wake, anapaswa kudumu hapo.

Na sasa, maono, jinsi ambavyo Bwana Mungu hutenda kazi pamoja nayo. Mimi . . .

⁶⁵ “Wakati Huyu, Roho Mtakatifu atakapokuja, Yeye atawafunulia mambo haya ambayo nimewaambia.” Sasa, hakuna haja ya kujaribu kuliwazia, kwa njia nyingine yoyote. Yeye ndiye Mwandishi. Hakika anapaswa kujua yale aliyoandika. Mnaona? Biblia ilisema Yeye aliliandika. “Hata watu wa kale, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, waliliandika Neno.” Basi kama Roho Mtakatifu ndiye Mwandishi wa Neno, hakika Yeye anajua jinsi ya kulifasiri vizuri kuliko tujuavyo sisi. Hebu Yeye alifasiri. Nanyi mnajua vipi, jinsi Yeye anavyolifasiri? Sasa, usiyakose mambo haya iwapo unakuja kwenye ibada ya uponyaji. Angalia. Usikose hili. Yeye analifasiri kwa njia gani? Kwa njia hii, kwa kulithibitisha, mnaona, kulifanya litimie.

⁶⁶ Hivyo ndivyo Yesu alivyosema. “Yachunguzeni Maandiko. Ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele; na Hayo Ndiyo yanayosema kwamba Mimi ni nani. Hayo Ndiyo yanayonena habari Zangu. Na ni nani anayeweza kunihukumu Mimi? Ni nani anayeweza kunihukumu kwamba nina dhambi?” *Dhambi*

ni “kutokuamini.” “Nisipozitenda kazi nilizoandikiwa Mimi, basi msiniamini. Lakini nikizifanya hizo kazi, wala hamwezi kuniamini, basi aminini hizo kazi, kwa sababu Ne—Neno lilisema habari zake.” Mnaona? Hayo ni akili ya kawaida tu, ya kila siku.

Sasa, Mungu, “Karama na miito havina majuto.” Tunajua Biblia inasema hayo. Wanafanya hivyo.

⁶⁷ Imekuwa yapata, karibu miaka miwili sasa. Nilikuwa... Asubuhi moja nilikuwa nikitembea nyu—nyumbani, na nilikuwa nimeketi kwenye kiti. Sasa, hili linaonekana la kigeni sana, kwamba Mungu angeweza kumjumuisha mnyama. Kama vile ndugu fulani wa thamani, kwenye lile ono la Mbinguni, ya kule kutwaliwa juu kudogo nilikokuwa nako; ninaamini niliwaambia kulihusu, wakati mmoja, ama mkutano fulani. Yeye aliniandikia barua hivi majuzi, na kusema... Sauti ya Wafanyabiashara lililiandika. Kasema, “Lilikuwa... ono lako lilikuwa sawa, Ndugu Branham, kuhamishwa kwako. Lakini, sikiliza, lilikuwa sawa mpaka uliposema farasi wako, ambaye wakati mmoja ulimpanda, alikuja akakiweka kichwa chake begani mwako.” Kasema, “Hakuna farasi Mbinguni, Ndugu Branham. Mbingu zilifanywa kwa ajili ya wanadamu, sio farasi.” Vema, nikawaza...

⁶⁸ Vema, kwa kawaida, ukiona mtu yeyote namna hiyo, inakubidi kuelezea kila kitu, wanajaribu tu kutafuta kitu fulani. Mnaona? Huwezi kumwelezea Mungu, kwa vyovyote vile. Inakubidi tu kumwamini.

⁶⁹ Lakini huenda likamfariji. Nikasema, “Ndugu, kamwe sikusema nilikuwa Mbinguni. Katika lile ono, niliuliza habari za Yesu, nao wakasema Yeye angali mbali zaidi ya hapa. Nilikuwa katika jimbo kama paradiso. Lakini, ili labda iweze kukusaidia, Biblia ilisema, katika Kitabu cha Ufunuo, kwamba, ‘Yesu alitoka katika Mbingu za mbingu, amepanda farasi mweupe. Nalo jeshi lote la Mbinguni lilikuwa likimfuata Yeye, juu ya farasi weupe.’ Kwa hiyo hapana budi kuna baadhi yao huko juu katika Mbingu za mbingu.”

⁷⁰ Mungu anajali kila kitu. Anajali mambo madogo ufanyayo, ama mambo makubwa ufanyayo. Anajali jinsi unavyolishughulikia kundi lako dogo, ama wewe jamaa mwingine unavyolishughulikia kundi lako kubwa. Anajali.

⁷¹ Wakati fulani uliopita ndugu yangu mwema, mwenye sifa, tulikuwa huko chini kwenye—kwenye... tukivua samaki mahali fulani. Nilikuwa nimeingia, kutoka mikutanoni, nikipumzika. Tulikuwa tukivua samaki kwa konokono, nasi tukavua lundo kubwa la samaki. Basi usiku huo tulikuwa tukiweka ugwe wetu mgumu wa kuvulia, ndipo tukaishiwa na chambo. Baadaye alasiri, nilitoka kwenda kuwavua mashavu ya samawati wadogo, jamaa hawa wadogo sana. Siwezi... Wale wakubwa unaweza

kuwala, lakini hawa ni samaki wadogo tu wa chambo. Basi nikaushtua ugwe, ugwe wa kuvulia, nilikuwa nikiwashika, nikiwatia kwenye ndoo.

⁷² Ndipo Kitu fulani kikanigusa, nikiketi kwenye mtumbwi huu. Mvulana huyu alikuwa ni Shahidi wa Yehova, naye ndugu yake alikuwa ndiyo kwanza tu aoko ke na kujazwa na Roho Mtakatifu, na kwa hiyo hao wavulana wawili walikuwa pamoja nasi. Basi wakati nikiwavua samaki hawa, sisi sote, Kitu fulani kilinigusa. Ndipo nikasema, “Mwajua, kutakuwako na kufufuliwa kwa uhai fulani, kama mnyama mdogo.” Vema, mnyama mdogo.

⁷³ Sasa, wengi wenu mnakumbuka kule kutabiriwa kwa Neno, lililosema, “Kutakuwako na mvulana mdogo atakayefufuka katika wafu, aliyekuwa amekanyagwa na motokaa.” Ndugu Jack Moore yuko pamoja nami usiku wa leo, ambaye alikuwa huko Finland wakati hilo lilipotukia. Mnaona? Wengi wenu hapa mnakumbuka nikiwaambia huku, mnaona, nikawaambia myaandike kwenye kitabu chenu. Angalieni.

⁷⁴ Naye Ndugu Wood akageuka, Ndugu Banks Wood, ambaye mvulana wake aliponywa, akiwa na polio. Ndipo akageuka akamwambia ndugu yake, “Angalia tu. Jambo fulani linakaribia kutukia.” Nikaendelea kuwavua samaki, mnaona. Kwa hiyo tukaweka ugwe wetu chambo cha samaki.

Usiku huo hatukushika chochote.

⁷⁵ Kesho yake asubuhi nilisema, “Kulikuwako na baadhi yao, wengi sana, mashavu ya samawati kule.”

⁷⁶ Akasema, “Aisee, jambo lingine, hivi hukusema kutakuwako na namna fulani ya kufufuliwa kwa uhai?”

Nikasema, “Naam.”

⁷⁷ Nawaambieni, nilipoondoka nyumbani, walikuwa... Msichana wangu mdogo... Kidogo sisi... Ninyi watu mnaweza kuwa nao mkiwataka, sasa, mnaona, bali mimi naogopa paka. Na kwa hiyo si—sipendi ile hisi ya kishirikina unayopata karibu nao. Na kwa hiyo hatunao nyumbani, na—nami ninaamini paka anaweza kutambua ya kwamba ninamwogopa. Kwa hiyo, baba yangu aliwaogopa paka. Kwa hiyo, basi, wasichana wangu wadogo walijua kutokuwa na paka wowote karibu na hapo. Basi maskini... .

⁷⁸ Msichana wangu mdogo akishuka kwenye kijia pamoja na msichana mwingine mdogo, basi alirudi, amehuzunika sana usoni, kisha akasema, “Baba?”

Nikasema, “Wataka nini, kipenzi?”

Akasema, “Jambo la kuchukiza sana limefanyika.”

Nikasema, “Ni kitu gani?”

Akasema, “Laiti tu ungalijua!”

Nikasema, “Vema, niambie.”

⁷⁹ Akasema, “Mtu fulani amemtupa maskini paka mzee, kwenye kijia hapa.” Kisha kasema, “Kitu hicho kiko karibu kufa, karibu hakiwezi kutembea.” Naye kasema, “Baba, unajali kama tukimlisha na kumhudumia?”

⁸⁰ Nikasema, “Hakika sijali. Kama mnataka kumlisha, iweni tu waangalifu. Msimwache awakwaruze.” Nikasema, “Hebu nimwone huyo paka.”

⁸¹ Kwa hiyo walipomleta huyo paka huku, nilichukua kasha, na, hakika, kesho yake asubuhi tulikuwa na lundo zima la vijipaka.

⁸² Ndipo basi, kwa hiyo, maskini—maskini mvulana wangu, nilipokuwa nikiondoka, mtoto Joseph, alikuwa akiwaangalia. Loo, alidhani walikuwa wanapendeza, mwajua, wakipanda huku, mwajua. Basi—basi anamshika mmoja mkononi mwake; kidogo akamfinya kupita kiasi, kisha akamwangusha sakafuni. Maskini jamaa huyo akaanza kugeuka, na kugeuka. Nikawaza “Loo, jamani!”

⁸³ Nami nikawaza, “Vema, sasa, huyo huenda akawa ni maskini huyo mtoto wa paka, nitakaporudi nyumbani.” Mnakumbuka kile kisa cha oposamu. Nikawaza, “Vema, huenda ikawa ni yule mtoto wa paka.” Kwa hiyo basi tulikuwa tumeketi nyuma katika ghuba dogo, tukivua samaki, nasi tulikuwa tukiwashika hawa wenye mashavu ya samawati wenye ukubwa wa wastani basi, tukiwarudisha wale wadogo.

⁸⁴ Ndugu Lyle, ndugu ya Ndugu Banks, alikuwa akivua kwa ufito wa kushtua, ndoana kubwa mno, na lundo kubwa la wadudu. Akamwacha maskini huyo shavu la samawati aimeze ndoana hiyo mpaka ndani ya maskini kijitumbo chake. Basi alipomvuta juu, alisema, “Sasa, laiti mngalitazama *hapo*,” yapata urefu *huo* tu. Naye akaninii tu...asingeweza kuitoa hiyo ndoana, nadhani. Hakuna njia nyingine; kuukata tu huo ugwe. Naye alitaka kuiokoa ndoana yake. Kwa hiyo akavuta tu mashavu, matumbo na kila kitu, kutoka ndani yake, namna *hiyo*, kisha akamtupa juu ya maji. Naye a—akatetemeka mara tatu ama nne akalala pale tu. Akasema, “Umepumua mara yako ya mwisho, jamaa mdogo.”

⁸⁵ Nikasema, “Lyle, anapoanza kuuma...Chukua ndoana ndogo kuliko hiyo. Wakati anapoanza kuuma, chukua ufito huu wa kuvulia ulio hapa, na mara anapoanza kuuma, mshike. Unaona? Kabla hajaiingiza ndani na kuimeza, mshike kinywani mwake.” Nikasema, “Huo ndio mchezo wa kuwashika.”

⁸⁶ “Aa,” akasema, “Ningevuta vibaya,” naye akaendelea tu. Naye akajaribu mara chache, na kukosa kama mara tatu ama nne. Ndipo akakiweka kitu hicho chini, kasema, “Nitamwacha tu aimeze tena.”

⁸⁷ Kwa hiyo samaki huyu mdogo akaelea hapo juu ya maji kwa muda kidogo, loo, nadhani, dakika thelathini. Ndipo mawimbi yakaanza kupanda na kuingia ndani.

⁸⁸ Nikasema, “Vema, itatulazimu kuondoka karibuni sana. Tuna ndoo sasa, kwa hiyo itatulazimu kuondoka.”

⁸⁹ Ndipo nikasimama, kumtupa kwenye majani-duara ya yungiyungi, nimvute. Kulikuwako na baadhi ya wenye tumbo jekundu kule nyuma. Kwa hiyo nikaanza, kuvuta cha—cha—chambo kutoka kwenye jani-duara, mnajua, nikairusha juu ya jani-duara, na kuivuta ghafla, kama vile ninyi jamaa na wanawake mnavyoyjua kuhusu kuvua samaki.

⁹⁰ Ndipo nilipoanza kufanya hivyo, mara ghafla, Kitu fulani kikashuka kupitia hivyo vilima, kama tu Upepo ukivuma. Na Hicho kikaenda juu yangu. Nikauangusha ufito, na kusimama katika huo mtumbwi. Ndipo nikaangalia kote. Nikasikia Sauti ikisema, “Unamwona yule samaki mdogo?” Naye huyo hapo, amelala pale.

⁹¹ Nikasema, “Unamwona yule samaki mdogo?” kama tu Yeye alivyolisema. Hapo maskini pezi zake ndogo zilikuwa zimekakamaa nje, naye alikuwa, amelala juu ya maji kwa nusu saa. Nayo Biblia hii ikiwa imefunguliwa sasa. Mnaona?

Ndipo Yeye akasema, “Nena naye, ukamrudishie uhai wake.”

⁹² Basi nikasema, “Ewe samaki mdogo, katika Jina la Bwana Yesu, ninakurudishia uhai wako.”

⁹³ Nao hao watu wamesimama, wakiangalia. Maskini samaki huyo akageuka mgongoni mwake, na huyo akaenda kupitia majini. Karibu wazimie. Lyle akanawa uso wake majini. Akasema, “Nitaamka baada ya kitambo kidogo.” Akasema, “Na—najua ninaota.”

Nikasema, “Huoti.”

⁹⁴ Na papo hapo wakati ule ule, nadhani nilikuwa, kwenye mstari wa maombi, na watoto thelathini ama arobaini wenye kifafa. Na jinsi Mungu angezunguka, kutoka kwa hao watoto wenye kifafa, na kumfufua samaki huyo mdogo, inaonyesha tu ya kwamba Yeye anajali kila kitu.

⁹⁵ Kwa nini atumie nguvu Zake kuulaani mtini, wakati kulikuwa na maelfu ya wenye ukoma nchini? Naye akawapita hao wenye ukoma akaenda na kuweka laana juu ya mtini, ndipo akasema, “Mtu asile kutoka kwako,” ndipo huo mtini ukanyauka. Akatumia nguvu Zake, akionyesha ya kwamba anajali miti. Anajali samaki.

⁹⁶ Anakujali wewe. Ananijali mimi. Naye anapendelea kuona Neno Lake likidhihirishwa, na Yeye anatutegemea sisi kufanya hivyo, kwa kuwa sisi ni mawakala Wake. Hakuna chochote ndani yetu. Ni Yeye; kujitolea wenyewe na kutembea pamoja na Yeye.

⁹⁷ Nikaona ono asubuhi hiyo. Nilimwona mnyama mkubwa amelala kando ya kilima. Loo, alikuwa na jozi kubwa mno ya pembe. Nilikuwa kwenye safari ya kuwinda katika ono hili, yapata saa nne ama tano mchana. Nami nikanyemelea kule na kumpiga risasi mnyama huyo.

⁹⁸ Ndipo basi nilipokuwa njiani nikirudi, dubu mkubwa sana mkali, akasimama anishambulie, ndipo nikampiga risasi.

⁹⁹ Ndipo basi nikawaona wakizichukua hizo pembe, na mkono mdogo ukanyoshwa na kuzishika hizo pembe, na kuweka utepe juu yake. Zilikuwa inchi arobaini na mbili, kutoka kwenye ncha ya mkalio hadi nchani mwa pembe, urefu wa inchi arobaini na mbili. Sijawahi kuona mnyama yeyote kama huyo, ncha kali mno zilizochongoka juu ya pembe yake. Na, hata hivyo, alionekana kama kulungu, bali ni, loo, jamani, angefanya kulungu wawili au watatu. Sijawahi kuona kitu kama hicho.

¹⁰⁰ “Vema,” nikasema, “labda litakuja kutimia siku moja. Nitaliandika tu.”

¹⁰¹ Nikaenda huko chini Kentucky pamoja na rafiki yangu, ndipo Ndugu Miner Arganbright akanipigia simu, kasema, “Ndugu Branham, una shughuli nyingi?”

¹⁰² Kasema, “Si sana.” Nikasema, “Nilikuwa kwenye ninii yangu...Ninayo majuma mawili sasa. Niko kwenye likizo ndogo.”

¹⁰³ Kasema, “Hima twende Canada, huko Alaska, pamoja nami. Tunataka kuunda tawi la Wafanyabiashara huko Anchorage na pia huko Fairbanks.”

Nikasema, “Linasiikika ni jema, kama ninaweza kupata wakati wa kufanya hilo.”

¹⁰⁴ Akasema, “Vema, Ndugu Branham, kama utafanya hilo, nitakwambia nini, tutakupa mawindo mazuri ya dubu mkubwa mkali.”

¹⁰⁵ Nikawazia, “Loo, hilo linasiikika ni jema.” Nikawazia, “Loo, loo, hilo hapo lile ono. Mnaona, hilo ndilo.”

¹⁰⁶ “Mawindo mazuri ya dubu mkubwa mkali,” nikasema, “hilo linasiikika zuri. Siendi kwa ajili ya hilo. Lakini, wakati tukiwa huko juu, na baadhi ya viongozi wanataka kunipeleka huko nje, bure, nitafurahia kwenda.”

Kwa hiyo, yeye akasema, “Vema, wa—watafanya hivyo. Tumeliandaa.”

Nikasema, “Vema, sasa ngojeni. Hebu niliombee jambo hilo.”

¹⁰⁷ Ndipo nikapanda kwenda mwituni siku hiyo, na kila nilipoomba, ndivyo nilivyoenda mbali, wakati wote, mbali kabisa nalo. Nikawaza, “Ajabu hiyo.” Basi siku mbili baada ya hapo, nikampigia simu Ndugu Arganbright. Nikasema, “La.”

¹⁰⁸ Yeye akasema, “Ndugu Branham, tunafanya maandalizi ya mambo.”

¹⁰⁹ Nikasema, “Msifanye hivyo. Roho Mtakatifu amelikataa.” Ndipo nikamwambia hilo ono. Nikasema, “Si—sijui, Ndugu Arganbright, lakini ni jambo geni. Ila Yeye hataniruhusu kwenda huko, na, hata hivyo, linasikika kama hapo—hapo pangekuwa ndipo mahali.”

Naye akasema, “Vema, sasa, sote tuko tayari kwenda.” Nami nikasema . . .

¹¹⁰ Sasa, wengi wenu watamwona Ndugu Arganbright. Yeye anakuja hapa sasa, kuandaa pamoja nami, kwenda ng’ambo baada ya mkutano huu. Na kwa hiyo mnaweza kumwuliza hadithi hiyo. Kwa hiyo tukasema . . .

Nikasema, “La. Siwezi kwenda. Roho Mtakatifu ananiambia nisiende.”

¹¹¹ Ni vema zaidi kutii, haidhuru ni kiasi gani, jinsi linavyoonekana ni zuri. Nitahubiri juu ya jambo kama hilo kesho usiku, Bwana akipenda. Kwa hiyo sasa, kumbukeni, haijalishi jinsi linavyoonekana ni zuri, kama Mungu hayuko ndani yake, kaa mbali nalo. Haijalishi linaonekana la madoido jinsi gani, kaa mbali nalo. Lina ufanisi jinsi gani, kaa mbali nalo ikiwa Mungu hayuko ndani yake. Kaa mbali nalo. Sasa tutalizungumzia hilo kesho usiku, Bwana akipenda.

¹¹² Sasa, basi nilipoenda nyumbani, Billy akaniambia, mwanangu, akasema, “Baba, unamjua yule mwindaji uliyeenda kuwinda pamoja naye msimu uliopita wa kupukutika majani huko juu, jina lake Southwick?”

¹¹³ “Loo,” nikasema, “juu kwenye . . .katika . . .chini ya Yukon kule?”

Akasema, “Naam.”

Kasema, “Yeye yuna barua hapa kwa—kwa ajili yako.”

¹¹⁴ Yeye ni Ndugu Eddie Byskal, ambaye ndiye kiongozi wa shi—shirika la wahudumu wa jimbo hilo la kaskazini magharibi kule juu, mvulana mzuri sana, huenda akawa hapa kwenye mkutano huu. Anapanga kuja huku wakati huu. Maskini mvulana mzuri, naye ana familia nzuri. Yeye ni—yeye ni mmishenari huko juu sasa kwa Wakrii, Wahindi Wakrii. Nami nilikuwa tu pamoja naye msimu uliopita wa majani kupukutika. Halafu basi . . . Ama, msimu wa kiangazi uliopita, hasa.

¹¹⁵ Ndipo yeye, Eddie, alitaka kunipeleka kwa Bud, ambaye alikuwa ni mmoja wa waongofu wake kwa Kristo. Mke wake alikuwa ni Mpentekoste hodari. Bud alikuwa mfuga wanyama, naye ndio kwanza tu aingie hivi majuzi. Lakini alikuwa amegawiwa, ambako waliwaondosha Wahindi na kuwaweka katika hifadhi, eneo zuri sana la kuwindia. Yapata sita . . .Loo,

nadhani ana yapata maili mia tatu mraba, ama zaidi, mle ndani, kwa ajili ya jimbo ambalo amegawiwa na serikali ya Canada.

¹¹⁶ Vema, msimu huo wa majani kuchipuka, nilipokuwa huko juu, tulienda kuwinda dubu baada ya mkutano, lakini wakati tuliponinii...katika Mei, lakini pepo za chinuku zikaja zikatukatilia mbali. Tulikuwa na yapata...Kamwe hakuwa amesikia lolote juu ya hiyo mikutano, naye Eddie akaendelea kumwelezea juu ya hiyo mikutano.

¹¹⁷ Ndipo akasema, "Humaanishi kuniambia kwamba, leo hii, kwamba Mungu anajionyesha Mwenyewe, na kuonyesha mambo yajayo kabla hayajatukia?"

Eddie akasema, "Hiyo ni kweli kabisa."

¹¹⁸ Kwa hiyo akaendelea kuzungumza nami. Akasema, "Unajua, ninaye ndugu aliye na kifafa." Kasema, "Laiti ungaliweza tu kumfikia ndugu huyo!" Kasema, "Ninaamini, kama kamwe ningaliweza kumpeleka kwenye mmoja wa mikutano yako, ninaamini angeponywa." Nikasema...Kasema, "Amekuwa nao maishani mwake mwote."

Nikasema, "Labda hivyo."

¹¹⁹ Vema, hakuuingii giza huko kwenye wakati huo wa mwaka, mwajua. Jua linashuka tu, na linakuwa...Loo, unaweza, wakati wowote, usiku wa manane, saa saba, unaweza tu kusimama, ulisome gazeti, chochote kile, unaona. Na yapata—yapata sehemu ya mwisho wa Mei jua kamwe haliteremki chini. Linainama kidogo sana, karibu lizame, yapata dakika kumi, kisha linarudi. Kwa hiyo tulilala tu chini wakati wowote tulipochoka.

¹²⁰ Halafu tulipokuwa barabarani tukitoka, tulikutana na kundi la Wahindi. Na, loo, nilimpata yule chifu mzee kule nyuma. Walimwacha akae kule kwa sababu alikuwa na watoto wawili. Hao huwazika watoto wao kwenye gogo, wapendwa wao. Namna fulani ya dini. Nao wanawaning'iniza mtini, kwa hiyo wakaiacha tu familia hiyo ikae pale. Jamaa mzee mzuri, amepita umri wa miaka tisini, ameketi kwenye matandiko yake vizuri tu kama mmoja wa wavulana wake.

¹²¹ Na kwa hiyo tukaondoka kesho yake. Yeye akasema, "Hakuna njia ya kuvuka sasa. Pandeni juu ya milima na namna hii." Loo, ilikuwa ni maili zingine mia moja, kutengeneza kijia. Kwa hiyo, tusingeweza kufanya hivyo. Muda ulikuwa umeenda sana. Tukaanza kurudi.

¹²² Basi tulipokuwa tukirudi, Bud ana msafara wa farasi wadogo, na baadhi yao walikuwa wamekwama kwenye kinamasi na kadhalika. Nami nilikuwa nikitembea pale, nikizungumza, na, mimi pamoja na Eddie. Naye Bud amempanda farasi aliyetangulia, akijaribu kutoka. Tulikuwa na farasi ishirini na mmoja. Nami nilikuwa nimemfunga mmoja kamba, nikamtoa

nje. Basi mara alipotoka nje, ndipo farasi wangu mwenyewe wa matandiko akaingia ndani. Nami huyu hapa, nikitoka nje kule. Basi nilikuwa nimejaa matope na kadhalika... Katika dakika chache, nikampanda farasi wangu, na kuyapangusa matope kutoka kwenye nguo zangu, namna *hiyo*, nikaanza kuondoka.

¹²³ Ndipo moja kwa moja mbele zangu, upande wa pili wa hicho kilima pale, akaja kijana mwanamume. Nikamwanguka. Nikarudi nyuma katika matandiko na kumsimamisha farasi wangu. Ndipo nikamwona akianguka katika kifafa, akibingirika tena na tena, na kutoa mapovu, naye akawa mkorofi sana, na kurarua tu kila kitu. Ndipo basi akatulia. Nikaona salamanda la siku nyingi. Nikaona shati lake likiungua.

¹²⁴ Eddie alikuwa yapata umbali wa nusu jengo la mji mbele yangu, akijaribu kumchukua farasi mwingine. Farasi huyo mdogo akakimbia akaondoka kwenye kijia, akaingia mle ndani, akijivua mizigo, akiruka nyuma. Kwa hiyo basi nikakimbia pale kwa Eddie. Tukamtuliza huyo farasi. Nikasema, "Eddie, ninalo BWANA ASEMA HIVI kwa ajili ya Bud."

Akasema, "Ndugu Branham, ilikuwaje?"

Nikasema, "Ono. Nilimwona ndugu yake."

Akasema, "Loo, mtafute."

¹²⁵ Nikasema, "Wasimamishe farasi. Nitamwendesha wangu kwa kasi niwatangulie, niwazunguke farasi hawa, nione kama ninaweza kuwapata na kuwazuia kando ya hiki kilima."

¹²⁶ Nikaenda mbio nikalizunguka lile genge, namna *hii*, pamoja na fa-... juu ya farasi wangu. Nikamsukuma juu, nikapanda kule juu. Ndipo nikaweka mkono wangu juu ya matandiko. Nikasema, "Bud?"

Akasema, "Naam, Ndugu Branham."

¹²⁷ Nikasema, "Nataka kukwambia jambo fulani. Ndugu yako..." kisha nikatoa sifa zake.

Akasema, "Naam. Ni nani aliyekwambia?"

Nikasema, "Hakuna mtu. Bwana ndio kwanza anionyeshe huyo."

Nikasema, "Utaniamini kama mtumishi Wake?"

Akasema, "Bila shaka, Ndugu Branham."

¹²⁸ Nikasema, "Tuma mtu," yapata—yapata maili mia nane kurudi kwenye ustaarabu, "mwambie ndugu yako aje huku. Na mara ya kwanza anapoanguka katika moja ya hivyo vifafa..." Nikasema, "Amekuwa na hivi tangu akiwa na umri wa yapata miaka miwili. Huenda usiliamini, bali ni vya kurithiwa. Babu yako alikuwa navyo."

Akasema, "Sasa, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli."

¹²⁹ Nikasema, “Sasa, wakati mvulana huyu anapokuwa na kifafa hiki, kutua shati lake kutoka mgongoni mwake na kulitupa motoni, useme, ‘Hili nafanya katika Jina la Yesu Kristo, kulingana na Neno Lake.’ Kamwe hatapata kingine, mradi tu ataamini.”

¹³⁰ Yeye aliinua tu mikono yake, akaanza kupiga mayowe. Akasema, “Sijawahi kuliona likifanywa, bali hakika uliniambia vile hasa ndugu yangu anavyofanana, na ukaniambia ukweli kuhusu babu yangu.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

¹³¹ Baada ya sisi kuondoka, alituma mtu akampata ndugu yake. Naye alikuwa akitoka kwenda kutengeneza kijia asubuhi hiyo, wakati alipokuja kwa basi (akija, linapitia hapo mara mbili ama tatu kwa juma, huku na huko kwenye barabara kuu ya Alaska), alikuja kule kwa . . .

¹³² Basi mke wa Bud, Lila, ni mtu tu mdogo sana, mwanamke mdogo, mkubwa kama mche wa sabuni ukiisha kutumiwa na familia kufulia. Mdogo tu . . . Yuna watoto watano, na maskini mwanamke mzuri sana.

¹³³ Basi Bud akatoka kwenda kuwaandaa farasi wake, maana anaenda kutengeneza kijia, tuweze kurudia hapo pamoja na wawindaji wake.

¹³⁴ Ndipo mara alipoondoka, vema, ndugu yake mle ndani, pasipo kutoa nguo zake nzuri bado, akashikwa na kifafa. Nao walikuwa wamepiga kambi kwenye kambi ya kale ya jeshi, ambamo Wamarekani, walipokuwa wakijenga hiyo barabara kuu, walikuwa nayo pale. Basi wakati . . . Walikuwa na maskini salamanda kubwa la kale kama jiko. Basi maskini Lila . . . Mvulana ali—alipatwa na kupaparika wakati aliposhikwa na hivyo vifafa. Naye alimwogopa kupita kiasi, naye angerukia dirishani, *kitu fulani ama kingine*, apate kuondoka. Lakini alipoanza kuruka nje, ndipo akawazia yale yaliyokuwa yamesemwa. Aliishakuwa katika mmoja wa hiyo mikutano, huko Dawson Creek.

¹³⁵ Akakimbia pale na kumtagaa jamaa huyu mkubwa, akakutua shati hilo kutoka mgongoni mwake, akilia, vifungo na kila kitu, shati lake jeupe, akaenda kwenye stovu, na kusema, “Hili nafanya katika Jina la Bwana Yesu, kulingana na Neno la Bwana tuliloambiwa.” Wala hajapata kushikwa na kifafa kingine tangu wakati huo. Hilo lilitosha.

¹³⁶ Yeye alikuwa ameagizia nje, mawindo ya bure. Nami sikuzote ninavitazamia vitu hivyo vya bure, mwajua. Kwa hiyo nikawaza, “Vema . . .” nikasema, “Nitaenda. Nitaona kama Bwana ataniruhusu kwenda.” Nikaomba. Basi mara nilipoomba tu, kila kitu kilianza kuelekea moja kwa moja upande huo.

¹³⁷ Nikamchukua Ndugu Fred Sothmann. Yeye yuko hapa mahali fulani mkutanoni. Uko wapi, Fred? Hilo hapo. Naam. Ni mmoja wa wadhamini wa kanisa letu. Ndugu Fred anajua ya kwamba hili lilisemwa miezi mitatu kabla halijatukia. Hiyo ni kweli, Ndugu Fred? Pia, nadhani, Ndugu Simpson. Ni wangapi walioko humu jengoni usiku wa leo wanaojua kwamba, kabla halijatukia, lilisemwa? Inueni mikono yenu. Haya basi. Na yalisemwa mbele ya kanisa, kile hasa ambacho kingetukia. Vema, sikujua huu kuwa ndio wakati.

¹³⁸ Kwa hiyo nikaenda kwenye—kwenye barabara kuu ya Alaska, naye Ndugu Fred akasimama kwa rafiki, waende wakawinde kongoni. Ni mbali mno kule kwa ajili ya kongoni. Kwa hiyo tuko huko juu kwenye maeneo ya kondoo, tulikokuwa tukienda. Na kwa hiyo sisi. . . Nilichukua ki—kipande cha—cha chaki ama tope, nikachora kwenye kizuizi cha upepo. Nikasema, “Sasa, Ndugu Fred, basi kama huu ndio wakati, utakumbuka vile hasa itakavyokuwa.” Naye anakumbuka.

¹³⁹ Nikapanda juu. Usiku huo tulipofika kambini, Bud alisema, “Ndugu Branham!” Akanikumbatia na kuruka juu chini, akinena kwa lugha na kupiga makelele, mwajua. Akasema. . . Na huyo, maskini kaoboi mkali, pia. Naye a—akimsifu tu Mungu. Akasema, “Unajua nini, Ndugu Branham? Ndugu yangu hajapata kifafa tangu wakati huo na kuendelea. Yeye ni mzima kabisa na mwenye afya, mwaka mmoja hapo kabla.”

¹⁴⁰ Nikasema, “Mradi tu ataliadini, litaendelea hivyo.” Ndipo nikasema, “Sasa mwambie ayatoe maisha yake kwa Kristo, na kumtumikia siku zake zote. ‘Nenda na usitende dhambi tena, la sivyo jambo lililo baya zaidi litakupata.’ Mnaona?” Nikasema, “Mwambie afanye hivyo sasa.”

¹⁴¹ Kwa hiyo nikasema, “Nina ono lingine,” nami nikamwambia juu ya ono hilo. Nikasema, “Sasa, kulikuwako na maskini jamaa fulani pamoja nami. Tulikuwa kwenye safari ya kuwinda. Walikuwa ni wanaume wadogo. Na mmoja wao alikuwa amevaa shati la kijanikibichi, la mirabamiraba.”

¹⁴² Naye akasema, “Vema,” akasema, “Ndugu Branham,” akasema, “Mimi sina shati la kijanikibichi, lenye mirabamiraba.” Mvulana wake, Blaine, mwenye umri wa miaka kumi na minane, kasema hana shati la kijanikibichi lenye mirabamiraba.

¹⁴³ Eddie Byskal, maskini mtu mwingine mdogo, mwenye uzito wa kama pauni mia moja na kumi, kasema, “Mimi pia sina, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Vema,” nikasema, “sasa, mnyama huyo. . .”

Akasema, “Alikuwa ni mnyama wa aina gani?”

Nikasema, “Alionekana kama kulungu.”

144 Akasema, “Hakuna kulungu hapa juu. Huku ni juu mno.” Akasema, “Labda alikuwa ni kuro.”

Nikasema, “Kuro ana paneli.”

Kasema, “Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Huyu alikuwa na pembe zilizochongoka.”

145 Akasema, “Vema, Ndugu Branham,” kasema, “tunaenda kwenye maeneo ya kondoo, sio maeneo ya kulungu au chochote namna hiyo.”

146 Nikasema, “Vema, labda ni kwenye safari nyingine. Ndugu Arganbright . . . Huenda ikawa ilikuwa ni Alaska mahali fulani,” nikasema, “maana ilikuwa ni dubu mkubwa mno, mkali.”

akasema, “Alikuwa ni dubu mkubwa mkali wa aina gani?”

Nikasema, “Mwenye ncha za fedha.” Huyu ndiye anayesifika sana miongoni mwao.

147 Akasema, “Mimi ni kiongozi. Nimekuwa kwenye misitu hii hapa maishani mwangu mwote. Sijawahi kuona mwenye ncha za fedha.” Kasema, “Nimemwona maskini dubu mkubwa mkali wa kawaida. Lakini,” kasema, “sijawahi kumwona mwenye ncha za fedha, sijawahi kumwona mmoja maishani mwangu.”

148 Nikasema, “Vema, wako, mmoja mahali fulani, nami nitampata.”

Akasema, “Nitasema hiyo ni kweli.” Akasema, “Nitasema hivyo.”

149 Tukaondoka, siku tatu baadaye. Tulifanya kambi huko juu kabisa, mwishoni mwa misitu.

150 Basi Mungu anisaidie, kama ikikaa hivyo mpaka kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, anijalie kuishi mle kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu. Ninapenda tu kuogelea kwenye maumbile hayo pale. Loo! Mtu yeyote asiyeweza kumwona Mungu kule, ni—ni kipofu, kiziwi, na bubu. Kumwona tu akijiakisi Mwenyewe katika milima hiyo mikubwa mno! Loo, jamani! Kilindi kinaita kilindi, basi, na tuko huko juu tukiwa tu na wakati mzuri.

151 Kwa hiyo tukapanda mlima mmoja. Inakubidi tu kutembea moja kwa moja, namna *hiyo*, upate kupanda juu. Loo, hakuna miti, kwa urahisi kuvumwani tu wa kongoni ndio unaona. Tuliona kondoo kama thelathini ama arobaini. Hakukuwako na yeyote aliyekuwa mkubwa vya kutosha kumchukua. Ilikuwa tu ni nusu mzunguko, na theluthi tatu mzunguko. Ni—nilitaka mmoja aliye mkubwa kutosha kutoka naye huko, ndio maana ya kurudi nyuma sana hivyo. Kwa hiyo sisi . . . nikashuka nikarudi.

152 Basi kesho yake tukaanza kuvuka, ndipo Eddie akaanguka majini wakati alipoanza kuruka avuke, amevaa jozi kubwa ya viatu.

¹⁵³ Huku tukipanda ubavuni mwa mlima, Bud alisimama na kusema, “Naomba nitumie darubini yako, Billy.” Nikampa darubini.

¹⁵⁴ Tungetembea kidogo, na kuzungumza habari za Bwana, na kupaza sauti, na kukimbia huku na huku kando ya kilima, tukiwa tu na wakati mzuri. Ni vema kwenda, safari ya kuwinda, ukienda pamoja na ndugu.

¹⁵⁵ Na kwa hiyo akaichukua darubini yangu. Akasema, “Ndugu Branham, yule pale kondoo dume wako. Kuna yapata wanane wa hao wamelala kama maili sita, pale pale juu ya kile kilele kingine. Hebu waangalie. Unawaona pamoja?”

Nikaichukua. Nikasema, “Nitasema, wale pale, kabisa.”

¹⁵⁶ Yeye akasema, “Vema, afadhali turudi chini, tuanze alfajiri yapata saa tisa.” Kasema, “Inatupasa kuwa kule ifikapo saa tatu, ama kuanzia saa nne. Maskini hao kondoo dume watakuwa wamelala. Huo utakuwa ndio wakati.”

Nikasema, “Ni vitu gani hivyo vingine vinavyotembea pale?”

¹⁵⁷ Akasema, “Hao ni kuro.” Nikasema . . . Kwa hiyo, umbali wa maili sita, mwajua, ni vigumu kujua wanavyoonekana.

¹⁵⁸ Halafu basi, tangu wakati huo na kuendelea, maili mia sita, jinsi kunguru arukavyo, hakuna hata ujia wala mkondo. Ndipo unapoifikia Pwani ya Magharibi, unaenda yapata maili mia nane hadi Vancouver, hakuna hata chembe ya ustaarabu. Ndipo ustaarabu unaofuata, ukienda *hivi*, ni Anchorage, yapata maili mia saba ama mia nane. Ukirudi *hivi*, unaingia kwenye ule mji mdogo, Yellowknife, ambako unapata meli pale yapata mara moja kwa mwaka kwa ajili ya Waeskimo. Ndipo, inayofuata, unaingia Urusi. Kwa hiyo, uko peke yako kabisa. Huko ndiko Mungu anapoweza kupumzikia, huko juu, kutokana na shida zetu zote na majaribu tunayomwingizia. Kwa hiyo mimi hupenda kwenda huko juu na kuzungumza na Yeye wakati akipumzika, unaona, kwa hiyo basi wakati kama vile ilivyokuwa jana usiku kwenye—kwenye kile chombo.

¹⁵⁹ Kwa hiyo tuliporudi chini, kisha kesho yake asubuhi tukaanza mapema. Kwenye yapata saa mbili, tulikuwa tumezunguka kwenye vichaka na kila kitu, mpaka tukakifikia kilele cha kilima. Ndipo tulipokuwa tukipanda, huyu hapa kuro jike mzee anaenda, na dume mzuri mkubwa. Akaenda, akaanza kupanda kilima, akiwa na paneli kubwa juu yake. Ndipo nikasema, “Vema, na kwa hiyo yule pale kuro wa kwanza niliyepata kumwona msituni, wa mwitu. Sijawahi kupanda juu hivi hapo kabla.”

Akasema, “Naam. Huyu ni kuro.”

¹⁶⁰ Kwa hiyo tukapanda juu ya kilima na kutazama. Kondoo hawakuwako. Kwa hiyo mimi na Bud tukatembea huko. Ndipo

Eddie akaanza kutoweka huko, na Blaine, mvulana wake, wakitafuta mawindo.

¹⁶¹ Nasi tukatembea hapa, na, loo, jamani, nikapaza sauti kwa shangwe, “Utukufu kwa Mungu!” Nikaangalia huko chini, na kulikuwako na hiyo milima mikubwa yenye vilele vya theluji; kuvumwani manjano ya kuro chini ya theluji. Na chini tu ya hapo inakuja isiyokauka, ambayo ilikuwa ni misonobari ya kijipse. Ndipo tukashuka chini kidogo, hapo kulikuwako na vichaka vya paa, vyekundu. Mbali kidogo na hivyo, kulikuwako na mpopla utetemekao, manjano. Yote ikiakisi kwenye ziwa chini yake. Loo, jamani!

¹⁶² Mimi na Bud tulikumbatiana tu, na kucheza tu dansi la yosayosa tukizunguka pale, tukipiga tu mayowe na kupaza sauti, na kumsifu Mungu. Ndipo tukaketi pale chini huku tumekumbatiana, na kumsifu tu Mungu. Basi tulikuwa na wakati mzuri sana, nadhani, kwa yapata saa mbili.

¹⁶³ Ndipo nikasema, “Aisee, sijui nini kilichompata Eddie?” Tulimwita “Mtanashati.” Kwa hiyo, tukarudi. Tukaanza kukivuka kile kilima. Nikasema, “Yeye asingeweza kupotea hapa juu.”

¹⁶⁴ Kisha kasema, “La. Blaine amerudi huko mahali fulani, naye ni Mhindi.”

¹⁶⁵ Kwa hiyo tukaangalia kote, ndipo nikaona kamera ya sinema imewekwa pale. Nikasema, “Hiyo ilikuwa ni ya Eddie.” Nikaangalia nyuma chini ya kilima. Ndipo nikaenda huko upande *huu*, naye akaenda upande huo mwingine.

¹⁶⁶ Naye Eddie alikuwa akifanya, “Sh-sh-sh-sh.” Alikuwa akinyemelea maskini yule kuro, wa kiume. Naye alikuwa akitaka kushuka pamoja naye, akawalishe marafiki wake Wahindi ambao alikuwa akiwafanyia umishenari. Kwa hiyo, akampiga risasi huyo kuro. Tukaenda chini na kumsafisha.

¹⁶⁷ Tukarudi, ni karibu saa saba. Tukawapata farasi wetu wa matandiko tena, yapata umbali wa nusu maili, walipokuwa wamesimama. Nasi tulikuwa tumesimama pale. Yeye akasema, “Ndugu Branham, ungetaka kutembea?”

Nikasema, “Hakika.”

¹⁶⁸ Akasema, “Kama tukiupanda mlima huu... Hao kondoo dume walienda upande *huu*, na kuingia kwenye lile shimo lingine pale, labda. Kama hawakwenda, walienda upande *huu* mwingine.” Kasema, “Hebu tumwache Eddie na hao wengine warudi, nao wapitie kwenye mkato huu *hapa*, na wamchukue farasi wangu wa matandiko na farasi wako wa matandiko, wambebe huyo kuro wampeleke kambini. Nasi tutatembea tupitie tu hapa juu na kupafikia mahali pale. Nasi tunapaswa kuingia yapata saa nne ama saa tano usiku wa leo.”

Nikasema, “Sawa. Tutafanya hivyo.”

¹⁶⁹ Kwa hiyo, tulikuwa tumesimama pale. Tulikula tu kopo la samaki-kibua, moja moja, kila mmoja wetu. Kisha tukazika chini ya kuvumwani, hawa samaki-kibua. Nayo mikate yetu, tulikuwa tumeiweka ndani ya mashati yetu, nasi tulitoa jasho mpaka yote ikawa katika bongwe moja kubwa. Lakini ilikuwa ni mizuri, wakati ukiwa na njaa. Na ni sawa. Kwa hiyo, tukasimama pale.

¹⁷⁰ Nami nilikuwa tu nikiangalia kote. Ndipo nikaangalia kupitia darubini. Nikasema, “Bud, angalia hapa. Ni kitu gani kile kule?”

¹⁷¹ Yapata umbali wa maili tatu, huyo hapo kuro amelala. Naye alikuwa ni wa kipekee. Hakuwa na paneli; alikuwa na pembe kubwa zilizochongoka. Nikasema, “Unakumbuka? Angalia hapa. Ile pale ile mandhari, vivyo hivyo hasa. Na pale amelala yule mnyama, vile vile tu hasa.” Nikasema, “Kuna jambo moja tu linalolizua lile ono, mtu fulani mwenye shati la kijanikibichi, lenye mirabamiraba.” Naye yule pale akasimama Eddie amevaa shati la kijanikibichi, lenye mirabamiraba. Nikasema, “Nilifikiri hukuwa nalo.”

¹⁷² Akasema, “Mke wangu hapana shaka aliliweka hilo kwenye mzigo. Nilipoanguka majini, jana, ilibidi, nibadilishe mashati.” Akasema, “Sikujua alikuwa ameliweka mle ndani, Ndugu Branham. Samahani nilikwambia jambo lisilo kweli.”

Nikasema, “Ilibidi tu ufanye hivyo, mwanangu.”

¹⁷³ Loo, Bud akaanza kupaza sauti. Akasema, “Unaweza kusimama papa hapa na kumpiga risasi, umbali wa maili tatu. Sivyo, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Kulingana na lile ono, nilikuwa karibu sana naye.”

¹⁷⁴ Akasema, “Ndugu Branham, ninakwambia, utafikaje kule?”

Nikasema, “Sijui mimi, bali nitafika kule.”

Kwa hiyo akasema, “Utaendaje?”

Nikasema, “Nitayazunguka mandhari haya.”

¹⁷⁵ Akasema, “Huo ni mwambatope.” Nami . . . Kasema, “Kama ukiteleza, utalaliwa na yapata tani elfu moja ya theluji, katika muda wa kama sekunde moja.”

¹⁷⁶ Na nikasema, “Bwana atalishughulikia hilo. Hivyo ndivyo nilivyoenda, katika lile ono, kuzunguka moja kwa moja.”

Akasema, “Vema, nitakufuata.” Huyu hapa anakuja.

¹⁷⁷ Nao wavulana hawa wakasema, “Tutakaa hapa sasa mpaka tuone ukimpata huyo kuro,” nao wakasema, “kisha tuta—tutashuka, tuwachukue farasi na kuingia mle. Tutakutana nanyi huko chini mwishoni mwa mpaka, yapata, loo, yapata maili nne au tano huko chini.”

Akasema, “Vema.”

178 Kwa hiyo tukaanza kuzunguka, mimi na Bud. Katika yapata nusu saa, tukazunguka moja kwa moja. Naye yule kuro amelala pale pale, akituangalia moja kwa moja, wala hakutuona. Hapana shaka alikuwa amelala. Basi tukavuka mkato mdogo, kisha tukarudi, na kupanda kufikia yadi thelathini kutoka kwake. Yule pale amelala. Mnyama huyu, mkubwa mno, akaamka kutoka pale, nami nikampata.

179 Ndipo tulipokuwa tumeketi pale, tukikata shingo, na kadhalika, kutoka kwake, namna hiyo, Bud alisema, “Hivi ulisema ya kwamba pembe hizi zilikuwa ni inchi arobaini na mbili?”

Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

180 Akasema, “Ndugu Branham, hazina budi kuwa ni mia moja na arobaini na mbili,” kichwa kikubwa mno.

Nikasema, “La. Ni arobaini na mbili hasa.”

Kasema, “Nina utepe wa kupima pale chini.”

Nikasema, “Kwani unalishuku?”

Akasema, “La, bwana.”

181 Akasema, “Lakini, ngoja kidogo, hivi hukuniambia ya kwamba utampata dubu mkubwa mkali kabla hujarudi chini? Kungekuwako na mwenye ncha za fedha, kabla hujarudi mahali yule mvulana alipokuwa, aliyevaa shati la kijanikibichi?”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

182 Akaangalia nyuma chini ya kile kilima. Vema, hakuna kitu juu *hivyo*, hakuna hata kidogo. Ni kuvumwani tu, yote unayoona, maili na maili, safu ya vilima vya kuvumwani tu. Yeye akasema, “Kwani yuko wapi, Ndugu Branham?”

183 Nikasema, “Yeye anaweza kuleta mmoja. Yeye alisema hivyo.” Nikasema, “Hivi unalishuku hilo, Bud?”

Akasema, “La, bwana.”

184 Vema, tukishuka kilimani, tulikuja namna *hii*. Angeibeba bunduki kwa kitambo kidogo, nami ningekibeba kile kichwa, kisha tunabadilishana. Inakubidi tu kutembea kwa upande, ukishuka chini, hizo pembe kubwa zikichoma tu kwenye kuvumwani. Ndipo tukafikia yapata maili moja kutoka kwake. Tukasimama na kuangalia kote. Akasema, “Maskini dubu huyo afadhali aanze kujitokeza, sivyo?”

Nikasema, “Una—unasumbuliwa na nini?”

Akasema, “Hakuna.”

185 Tukaendelea hata tukaufikia mto mdogo wa barafu ukipitia pale. Tukaketi chini pale tukapata baridi kidogo. Yeye akasema, “Ndugu Branham, wazia tu hilo,” kasema, “hatuna zaidi ya kama, loo, chini ya nusu maili kufikia walipo wale wavulana,

na mahali fulani kati ya hapa na pale utamwua dubu mwenye ncha za fedha.”

¹⁸⁶ Nikasema, “Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.” Akasema... Nikasema, “Unatilia hilo shaka, Bud.”

¹⁸⁷ Akasimama na kunishika mkono. Akasema, “Ndugu Branham, ndugu yangu kamwe hajapata kifafa tangu siku ile hadi wa leo.” Akasema, “Mungu yule aliyeweza kukwambia juu ya ndugu yangu, asingeweza kukudanganya.”

Nikasema, “Bud, atakuwapo.”

Akasema, “Atatoka wapi?”

¹⁸⁸ Nikasema, “Sijui, lakini,” nikasema, “Bud, nina umri wa miaka hamsini na miwili,” (wakati huo), nami nikasema, “nimeona maono, tangu nilipokuwa mtoto. Nami nilipomwona huyu kuro hapa, ameuawa, nawe utaona kama pembe zake si inchi arobaini na mbili. Halafu basi, ono lile lile, nikienda zangu kurudi mahali wale wengine walikuwepo, niliokuwa nao, nilimwua huyu mwenye ncha za fedha, dubu mkubwa mkali.”

Akasema, “Ndugu Branham, ninaweza kuona umbali wa maili ishirini.”

¹⁸⁹ Akasema, “Itambidi Mungu kumvuta kutoka ardhini, ama kumshusha chini kutoka angani, ama kitu fulani.”

Nikasema, “Usiwe na wasiwasi. Atakuwapo.”

¹⁹⁰ Tukaenda yapata yadi zingine mia moja. Alikuwa karibu tu amechoka pia. Hii ilikuwa na uzito wa karibu ratili mia moja na hamsini, nyara hii. Kwa hiyo, tukishuka kilimani, basi a—akaiweka chini. Akasema, “Whiu! karibu nikate tamaa.”

¹⁹¹ Nikasema, “Naam.” Tukafikia kwenye mbilikimo, misonobari mbilikimo midogo basi, yapata urefu *huo*. Kulikuwako na kware wachache wakiruka huko, na kulikuwako na kware wa kike wenye manyoya miguuni, na kwa hiyo nikawatupia mawe namna hiyo.

Kwa hiyo akasema, “Umewahi kula mmoja wa hao kware wenye manyoya miguuni?”

Nikasema, “La. Siamini nimewala.”

¹⁹² Akasema, “Hao ni watamu. Ni watamu tu kama hao kware.” Akasema, “Ndugu Branham?” Akatoa maskini kofia yake kubwa nyeusi, akajipepete. Kasema, “Ni karibu wakati ambapo maskini dubu huyo anapaswa kujitokeza, sivyo, jamani?”

Nami nikasema—nikasema, “Bud, unalitilia hilo shaka.”

¹⁹³ Akasema, “La. Silitili shaka. Lakini, Ndugu Branham, si—si—siwezi tu kuelewa.”

¹⁹⁴ Nikasema, “Wala na mimi. Si juu yangu kulielewa. Ni juu yangu kuamini.” Amina. Mungu Mbinguni anajua mambo haya

ni kweli. Hivi ningesimama hapa na kusema hili, kama halikuwa ni kweli?

¹⁹⁵ Ndipo nikaanza kugeuka, nimpe bunduki, nami nikichukue kile kichwa. Basi wakati nikigeuka, nikasema, “Bud, una ile darubini shingoni mwako. Ni kitu gani kile kimesimama kule kando ya kile kilima?”

¹⁹⁶ Basi akainua ile darubini upesi. Akasema, “Loo, naomba heri,” kasema, “kama si ng’ombe wa maziwa wa mtu fulani!” Hakuna kitu kama hicho nchini. Kasema, “Huyo ndiye dubu mkubwa mno mkali niliyepata kumwona maishani mwangu. Na kwa hiyo naomba heri, hebu liangalie lile jua la manjano likimwanzia. Yeye ni mwenye ncha za fedha.” Kasema, “Waweza kusema yuko umbali gani?”

¹⁹⁷ Nikasema, “Yuko umbali wa kama maili mbili huko juu.” Nasi tulikuwa karibu tumechoka kabisa. Akasema . . . Nikasema, “Tunangojea kitu gani? Hebu twende.”

Naye akasema, “Una hakika ya kumpata?”

Nikasema, “Hakika nitampata.”

Akasema, “Hiyo ni bunduki gani unayotumia hapo?”

¹⁹⁸ Nikasema, “Sasa, usijali kuihusu hiyo.” (Ni maskini bunduki ndogo ndugu fulani alinipa kwenye mkutano wakati mmoja, miaka kadhaa iliyopita.) Basi nikasema . . . (Maskini .270, rahisi.) Ndipo nikasema, “Vema. Nina ninii . . . Mimi . . . Itatendeka.”

¹⁹⁹ Tukaendelea kukaribia. Na kadiri tulivyokaribia, ndivyo huyo dubu alivyoonekana kuwa mkubwa zaidi. Loo, alionekana kama lundo kubwa mno la nyasi kavu limewekwa pale kwenye kuvumwani ile, mwajua. Amesimama, kitu kinene, kikubwa, kikubwa mno, kichwa kipana *hivi*, mwajua, na taya zikitokeza nje, nyayo kubwa mno. Naye alikuwa akiyachakura matawi haya madogo ya miforsadi, namna *hiyo*, mwajua, akiyala. Naye amejikakamua kabisa, jamaa mkubwa mno! Tukafikia yapata, loo, yapata yadi mia nane kutoka kwake.

²⁰⁰ Akasema, “Hey, Ndugu Branham, u—uliwahi kumpiga risasi dubu mkubwa mkali hapo awali?”

²⁰¹ Nikasema, “Nimewapiga risasi dubu wengi, Bud, ila kamwe sijawahi kumpiga risasi dubu mkubwa mkali mwenye ncha za fedha hapo awali.”

²⁰² Akasema, “Unajua, mwenye ncha za fedha ndiye mpiganaji mkubwa kuliko dubu wote.”

Nikasema, “Naam, ninaelewa hilo.”

Akasema, “Yeye hajui jinsi ya kufa.”

Nami nikasema, “Kwa hiyo?”

²⁰³ Akasema, “Usininii . . . Una—una—una umbali gani? Inakubidi kumkaribia kiasi gani ukiwa na hiyo?”

²⁰⁴ Sasa, hebu mwulizeni tu. Mwandikieni barua. Nitawapa anwani yake. Yeye alisema, “Hebu mtu yeyote aniandikie juu yake, atakaye, juu ya yoyote ya mambo hayo. Acha niwaambie mimi.” Na kwa hiyo. . .

Basi nikasema, “Kwa hiyo?” Nikasema. . .

Akasema, “Sasa?”

²⁰⁵ Nikasema, “La, la. Nilikuwa karibu kuliko hivi, Bud. Nilikuwa karibu sana, karibu naye.”

²⁰⁶ Akasema, “Tunakaribia sana sasa. Anaweza kushambulia wakati wowote.”

²⁰⁷ Nikasema, “Najua hilo. Lakini,” nikasema, “Bud,” nikasema, “itakuwa sawa.”

²⁰⁸ Akasema, “Sasa, unapompiga risasi dubu,” kasema, “sasa, Ndugu Branham, unampiga risasi upande wa nyuma. Inakubidi kumvunja, maana ataendelea kupiga vita, ndiposa hawezi kuinuka.”

Nikasema, “La, kulingana na ono, nilimpiga risasi moyoni.”

Akasema, “Natumaini hukufanya kosa juu ya hilo.”

²⁰⁹ Nikasema—nikasema, “Sikukosea.” Nikasema, “Ninakumbuka hilo.” Maana, katika—katika ono, wewe uko katika—uko katika dhamira moja, na zote mbili, kama tulivyoelezea hivi majuzi usiku. Uko katika mbili. Huwezi kusahau. Unaona? Kwa hiyo hivyo ndivyo ilivyo.

²¹⁰ Kwa hiyo tukaingia tena, yapata—yapata yadi mia mbili na hamsini. Hilo lilikuwa tu ndilo korongo la mwisho tulilovuka. Ndipo nikasema, “Hiyo karibu imetoshwa sasa. Mwangalie. Yeye si ni wa kupendeza?”

Akasema, “Naam, nadhani anapendeza.”

²¹¹ Ndipo—ndipo nikasema, “Vema, Bud. Sasa nitakaposimama kutoka hapa, yeye yuaja.” Kisha nikasema, “Angalia tu.”

Naye akasema, “Nitakuwa nikiangalia.”

²¹² Kwa hiyo nikaweka risasi kwenye mtutu wa hiyo bunduki, mwajua. Nasi tulikuwa hapo chini ya maskini korongo hili. Wakati tu niliposimama, huyu hapa akaja. Jamani, jamani! Nikasimama, nikafyatua risasi, na ilisikika tu kama ni bastola ya njegere imempiga. Jamani, hata haikumpunguzia mwendo, kwa vyovyote. Na, jamani, kabla. . .

²¹³ Nena kuhusu mbio! Sijawahi kuona kitu chochote kama hicho. Yeye, wangemshinda farasi mbio, kulungu, ama chochote kile, mwajua, dubu anaweza, namna hiyo. Yeye akitelemka moja kwa moja chini ya kilima hicho, moja kwa moja akituelekea, namna hiyo.

²¹⁴ Na mimi, kabla sijaweka risasi nyingine kwenye bunduki, alianguka akafa, yapata, loo, yapata yadi thelathini, arobaini

kutoka kwangu, akapinduka tu mwisho kwa mwisho; tukatoa moyo, mapafu, na yote, kutoka kwake. Ilikuwa ni risasi ya Nosler, ninyi mnaotumia bunduki mnajua. Kwa hiyo i—ilimlipua, naye akabingirika.

²¹⁵ Bud, akisimama pale, aliangalia kote, alikuwa mweupe kabisa mdomoni. Akasema, “Ndugu Branham, sikumtaka pajani mwangu.”

Nikasema, “Wala na mimi.”

²¹⁶ Akasema, “Whiu.” Kasema, “Nataka kukwambia, baada ya haya yote kwisha, jamani. Kama hiyo isingalikuwa ni moja ya hayo maono, nami nilikuwa nimeyaona yakitukia hapo kabla, kamwe nisingalikuja huku juu, karibu hivyo na dubu huyo, pamoja nawe.”

²¹⁷ Wala hakuna mmoja wetu angaliweza kumsukuma. Alikuwa na uzito wa karibu ratili elfu moja, nadhani, hivyo, jamaa mkubwa mno, mnene. Tusingeweza kumwosha, tulipata... tulimchinja. Tukaanza kushuka. Nasi tukasema... “Ndugu Branham?” Tukazichukua pembe. Akasema, “Kama pembe hizo zina urefu wa inchi arobaini na mbili kamili,” kasema, “Nitashikwa tu na mshtuko wa ghafla.”

²¹⁸ Nikasema, “Afadhali ushikwe nao sasa hivi, basi, maana hivyo ndivyo zilivyo.”

²¹⁹ Akasema, “Sijawahi kuona ni—ni—ninii... Inaonekana kwangu kama ninaota hili.”

²²⁰ Basi tulipofika kule chini, nami ni—nikamwambia Eddie, nikasema, “Sasa wewe angalia. Blaine ataweka mikono yake.”

²²¹ Sasa, mnakumbuka, kulikuwako na mkono mdogo kwenye zile pembe. Unakumbuka, Ndugu Fred, jinsi nilivyowaambia ingekuwa?

Basi nikasema, “Wewe angalia hilo,” kwa Eddie.

Na kwa hiyo Bud akasema, “Ngoja.” Akampeleka farasi wake pale.

²²² Nasi tulikuwa na dubu, mwajua, nao hao farasi wakirarua tu kila kitu. Mnajua jinsi wafanyavyo wanaponusa dubu mkubwa mkali ama dubu wa aina yoyote. Kwa hiyo ni—nikaenda pale, nikashika, nikijaribu kumshika farasi, yule farasi wa matandiko akijaribu kutoroka.

²²³ Basi akaenda kule akachukua utepe wake wa kupimia, kisha akaja akitembea pale, akiniangalia, namna *hiyo*. Kasema, “Njoo hapa, Blaine.” Nikampiga Eddie. Akauweka chini kwenye hii. Amina. Na basi anisaidie, inchi arobaini na mbili, kikamilifu kabisa!

²²⁴ Sasa, hizo pembe husinyaa karibu inchi mbili zinapokauka. Huyo dubu mkubwa mkali amewekwa kwenye chumba changu cha kusomea, nazo pembe zimetundikwa ukutani. Mrudishaji

sura alikuwa ameziandaa, na kuzitengeneza. Kuna utepe wa kupimia unaoning'inia kwazo, inchi arobaini na mbili, kamili.

225 Sasa, kwa nini Mungu amwambie mtu kitu kama hicho, kuhusu safari ya kuwinda?

226 Niliporudi, mama yangu alikuwa ni mgonjwa. Nikaenda kumwona. Akasema, "Billy?" Mnaona, Yeye alikuwa akinitia moyo, akiniandaa kwa ajili ya jambo fulani.

Nikasema, "Mama, Bwana sikuzote amekuponya."

Akasema, "Billy, ninaenda Nyumbani kumwona baba."

"Loo," nikasema, "mama, usizungumze namna hiyo."

Kasema, "Naam, ninaenda." Nikamwomba.

Naye Ndugu Fred na hawa mashahidi wote wanaoketi hapa wanajua.

227 Ndipo, jambo la pili mwajua, walikuwa wamemweka hospitalini. Daktari hata hakujua kilichokuwa shida yake. Vema, nikatoka nje kwenda kumwomba. Akasema, "Mwanangu, ninaondoka." Na sasa, mama yangu kwa namna fulani alikuwa ni mwanamke mwenye nguvu, hata hivyo.

228 Siku moja, siku kadhaa baada ya hapo, niliingia. Alikuwa amesimama pale, akiangalia moja kwa moja kuelekea Mbinguni. Akasema, "Billy, ninakuona."

Nikasema, "Mbona, hakika, mama." Kasema, "Ninakuona papa hapa."

229 Akasema, "Loo, wewe ni mzee sana, Bill," kasema, "nywele zako zenye mvi na ndevu zinaning'inia tu pamoja. Umeukumbatia msalaba, ukininyooshea mkono." Nilikuwa na fununu nzuri basi, ilikuwa imekwisha.

Sasa, ninyi ndugu hapa mnajua hilo kuwa ni kweli.

230 Siku iliyofuata ilikuwa ni Jumapili. Nilikuwa nikihubiri. Wakanipelekea ujumbe, "Nanii yako. . ."

Nikasema, "Siamini ya kwamba mama anatuacha. Mungu daima hunionyesha, watu wangu wakituacha. Lakini, mama, Yeye kamwe hajanionyesha mimi lolote kulihusu." Huu hapa ujumbe unaingia. Nami nilikuwa moja kwa moja katikati ya Ujumbe wangu, namna hii. Mtu fulani akaingia, kasema, "Nenda, nenda kwa mama yako sasa hivi. Mpigie simu. Yeye yuafa, kwenye dakika hii."

231 Nikasema, "Mauti, mshikilie kimya. Neno la Mungu ni muhimu sana kuliko hayo."

232 Mtu huyu anayeketi papa hapa, Ndugu Borders. Baada ya ibada kwisha, nilitoka nikaenda kumwona mama yangu. Nikakutana na Ndugu Borders. Akasema, "Ndugu Branham, wewe hujafikia urefu wa futi sita, bali nilimwona mtu mwenye urefu wa futi kumi amesimama mimbarani asubuhi ya leo."

Nikasema, “Ndugu Borders, Mungu atayashughulikia hayo yote kwa ajili ya mama.”

²³³ Basi siku chache baada ya hayo, wakaniita huko chumbani, na kweli yeye alikuwa anaondoka. Nikawakusanya watoto, tukasimama kukizunguka kitanda. Nikasema, “Mama, kweli unatuacha?”

Akasema, “Naam.” Kisha asingeweza kuzungumza tena.

²³⁴ Nikaendelea kumwambia, “Yesu anamaanisha nini kwako, mama?” Ninakumbuka nikimbatiza katika Jina Lake, muda mrefu uliopita, huko majini. Nikasema, “Niambie kile Yeye anachomaanisha kwako sasa.”

Akasema, “Zaidi ya uhai kwangu.”

²³⁵ Nikasema, “Mama, endapo unatuacha, mimi ni mvulana wako, yule...mhubiri. Ninataka kujua, kutoka kwa mama yangu mwenyewe ambaye anaenda kukutana na Mungu. Ninataka kuushika mkono wako hapa, mama.”

Kasema, “Ninataka ufanye hivyo.” Nikaendelea kuushika.

²³⁶ Asingeweza kuzungumza. Ilionekana kana kwamba alikuwa akilemaa, uso wake. Nikasema, “Hivi huwezi kuzungumza tena, mama?” Asingeweza kufanya...Nikasema, “Sikiliza. Hivi Yesu angali ni yeye yule kwako?” Angetikisa kichwa chake.

²³⁷ Ndipo akafikia mahali asingeweza kukitikisa kichwa chake tena. Nikasema, “Mama, hivi Yesu ni kila kitu kwako sasa? Yeye anakuja kwa ajili yako, katika dakika moja. Kila kitu, kwako?” Asingeweza kusogea.

²³⁸ Nikasema, “Mama, una kitu kimoja tu, wewe...Ninaona unayapepesa macho yako. Kama Yesu angali anamaanisha vile vile kwako kama alivyokuwa sikuzote, ile siku niliyokubatiza majini, pepesa macho yako haraka sana.” Akayapepesa macho yake, huku machozi yakitiririka chini, namna *hiyo*.

²³⁹ Ndipo Upepo mdogo ukaja, ukiingia humo chumbani. Mama akaenda Nyumbani.

²⁴⁰ Nikaja nyumbani, nikatoka nikaenda kwenye nyumba ya mazishi, nikachukua nguo. Loo, mnajua jinsi ilivyo. Imewabidi kufanya jambo lile lile. Watoto wote wakilia, mmoja chini mahali pamoja, na mmoja, pengine. Nikasema, “Mama alikuwa ndiye nguzo ya kuunganisha. Kamwe hatutakuwa vile vile tena.” Doc na familia yake kwenye kona *hii*. Jesse na familia yake kwenye kona *ile*. Ndio kwanza tumzike Howard, hivi majuzi. Nikasema, “Vema, tumekwisha, jamani.” Nikasema, “Tutaninii...Hatutakuja kuonana mmoja kwa mwingine. Mama alikuwa ndiye ngome yetu.” Nikasema, “Hatutaonana sisi kwa sisi, sio mara nyingi sasa.”

²⁴¹ Nikaenda nyumbani, usiku, tukiisha kuzichukua nguo zake. Nikapanda kwenda nyumbani.

²⁴² Bibi D'Amico, kuna mtu yeyote anayemjua, kutoka Chicago? Amekuwa rafiki mwema sana wa kampeni. Alikuwa amenipa Biblia. (Samahani.) Nayo ilikuwa ni moja ya hizo Biblia zenye herufi nyekundu pamoja na zipu. Pia mtu fulani, wakati nilipohubiri lile somo, *Mwana-Kondoo Na Hua*, walikuwa wamenitumia hua wawili, kama kishikizo. Ndugu yangu mwingine, Ndugu Norman, alikuwa amenitumia hua mdogo, na mwana-kondoo, Ndugu yangu Borders akanipa mwana-kondoo. Nikaichukua hiyo Biblia. Meda alikuwa hapo kwenye kona moja, analia.

²⁴³ Nanyi Wafanyabiashara wote hapa mnajua, nilipokuwa Jamaica, nilimwona mama mkwe wangu, nikawaambia mezani huko Jamaica. Nikasema, "Mmoja wa watu wangu yuafa, ambaye hana meno yoyote. Mimi huwaona wakiondoka." Papo hapo mezani, Demos Shakarian na hao wote wameketi pale. Saa chache kutoka hapo, mama mkwe wangu karibu aanguke afe, wakati mmoja, mnaona, hana meno, vivyo hivyo hasa.

²⁴⁴ Nikasema, "Nilimwona kijana mwanamume akitema damu." Nikapiga simu, kasema, "Msimwache Billy. . ."

²⁴⁵ Kuna mtu yeyote hapa aliyekuwa huko—huko kwenye mkutano wa Jamaica kule wakati huo huko—huko Jamaica, Kingston? Siwezi kuona. Naam. Kunao wawili. Kwa hiyo basi. . .

²⁴⁶ Ndipo nikasema, "Haina budi. . . Billy, usiende juu kule. Nimemwona jamaa mdogo akitema damu." Na ilikuwa ni shemeji yangu. Alienda, alikuwa na kutokwa na damu wakati mama yake alipofariki. Lilimtupilia tu kwenye mshtuko mkubwa mno.

²⁴⁷ Halafu nikisimama hapa siku hiyo, niliitwaa Biblia hii. Nikasema, "Baba, sijui. Labda ni upendo Wako tu, hukunionyesha yeye akituacha. Lakini nimevurugika sana, Mungu. Waweza tu kunipa neno la faraja kutoka kwenye Neno Lako?" Nikasema, "Jalia tu nisome jambo fulani litakalofariji, la kunifariji mimi." Nikaiacha tu Biblia ifunguke namna *hiyo*. Hiyo hapo, herufi kubwa nyekundu, "Hajafa, bali amelala usingizi." Ndipo nikaingia chumbani. Tukaenda kulala.

²⁴⁸ Yapata saa mbili, kesho yake asubuhi, nikaamka. Walikuwa wanaenda kumwandaa, yapata aduhuri, kwa hiyo tukashuka tukaenda kumwona. Meda akatoka nje kuwaletea watoto kiamshakinywa, naye mtoto Joe analia. Becky kwenye kona moja, angali analia, "Hivi nitawahi kumwona nyanya tena?"

²⁴⁹ Nikasema, "Naam. Naam. Utamwona. Yeye yuko tu ng'ambo ya pili, alipaa juu." Nikasema, "Yeye, tutamwona tena." Naye aliwapenda hao watoto wadogo, mwajua.

²⁵⁰ Basi, kwa hiyo, nao wote walikuwa wakilia, "Tunaweza kumwona nyanya alasiri ya leo?"

251 Nikasema, “Mnaweza kuuona ule mwili alimoishi, bali nyanya ameenda kuwa pamoja na yule nyanya yenu mwingine, hao huko juu Mbinguni.”

252 Naye Joe asingeweza kuelewa hilo, mvulana wangu mdogo, mwajua. Asingelielewa tu kabisa. Akasema, “Basi nyanya atashuka arudi usiku wa leo?”

253 Ndipo nikasema, “La, la. Sijui wakati atakaporudi. Yesu atakapokuja, yeye atarudi.”

254 Na nilikuwa nimesimama pale. Ndipo nikageuka, nikatembea chumbani. Basi nilipofanya hivyo... Msiniombe nilielezee. Hakuna njia ya kuelezea. Nilijiona nimesimama huko nje, kama tu ninavyoonekana kwenye kusanyiko hili. Na nilikuwa nikiongoza nyimbo. Kamwe sikufanya hivyo. Hata siwezi kuimba, hata kidogo. Kwa hiyo, na kulikuwako na umati mkubwa, mkubwa mno wa watu.

255 Upande *huu*, ju—jumba la mikutano lilionekana kana kwamba lilikuwa nje, kitu kama hicho, loo, sijui jinsi ungeliliita, kidogo chini ya kilima, na kidogo kama uwanja mduara. Na ulikuwa huko nyuma kabisa, hiyo mistari ilikuwa, mpaka ilibidi iinuliwe namna *hii*, kwa hiyo wale waliokuwa mbali kabisa huko nyuma iliwabidi kuangalia upande *huu*. Lakini wote moja kwa moja katikati... Safu tatu tu, namna *hii*. Na papo hapo katikati kulikuwa na kitu kama safu zimelundikana, za watoto wadogo wenye vifafa, watoto waliotemaa wamewekwa kwenye safu hizo.

256 Na nilikuwa na suti nyeusi, nami nilikuwa nikiimba, “Waleteni, waleteni, waleteni watoto wadogo kwa Yesu.” Tunauimba huo kanisani, sana, hasa sana katika kuwaweka watoto wakfu. Basi kulikuwako na, kitu kama sa—sanduku hapa, ambapo watu mashuhuri waliketi, nayo mimbara ilikuwa karibu na hapo. Lakini nilikuwa chini, nikiongoza nyimbo. Ndipo mara ghafla, mimi nikisimama pale, nikijiangalia mwenyewe, ndipo... Loo, usijaribu kuliwazia, maana huwezi. Ndipo wakati nilipokuwa *hapa*, ndipo ikawa ni *hapa*. Sijui. Wawili wao walienda pamoja. Na ni...

Hilo ni jambo jema wakati wawili wako wanapoenda pamoja.

257 Nilichukua kamera huko juu. Nikishuka, sikujua jinsi ya kupiga picha. Nikaangalia kupitia kwenye kitu hicho, na, jamani, ningeweza kuona vitu vitano ama sita mbalimbali. Kwa hiyo nikaanza kuifokasi. Billy aliniambia, kasema, “Iweke fokasi, ndipo vyote vikawa kimoja.”

258 Ni wazo zuri kufanya hivyo, mwajua. Unaona mambo tofauti ukianza kuweka fokasi. Basi tumia Neno la Mungu kumweka Yeye fokasi, nawe uta—utaona kile ninachozungumzia. Lakini liweke fokasi, kwanza, unaona.

259 Kwa hiyo nikisimama pale, nikiangalia, basi niliingia katika ono hilo. Na wakati nikiwa mle ndani, nilimwona mtu anayejulikana sana akirudi nyuma ya mahali hapo. Nao walikuwa... Nikasema, “Vema, wanakuja kwenye sehemu ya kijisanduku cha watu mashuhuri.” Kwa hiyo wakaja wakipanda juu *hivi*. Nami nikawaza, “Vema, nitaimba mara nyingine tena wakati mama huyo anapokuja.” Alikuwa amevalia mtindo wa kale.

260 Sasa, baadhi yenu enyi kina mama mtakumbuka hili, wakati walipovaa sketi, kitu kama hicho, kuzungushia *hapa*, nayo ikaenda chini sana juu ya viatu vya kamba. Nao walikuwa kidogo na ninii kamili... Mnaviitaje vitu hivyo, kama—kama vile mama huyu amevaa *hapa* sasa? Hiyo blauzi. Blauzi, moja ya vitu hivyo namna hiyo, nayo ilikuwa na mikono mirefu halisi ndani yake. Mnazikumbuka hizo? Nayo ilizunguka shingo *hapa*, pamoja na kitu kama kifungo kidogo kilichoingia *hapa* ndani. Halafu, amevaa kofia kubwa mno, imeinuliwa upande mmoja. Nao kina mama, siku hizo, walikuwa na nywele ndefu. Kwa hiyo wakaivuta chini namna *hii*, na kuweka kofia juu yake, na kuifunga kwa pini, mwajua, isije ikaanguka, kwa kuwa iliwabidi kupanda farasi miguu ikiwa ubavuni na kadhalika.

261 Kwa hiyo mama huyu alikuwa akija juu, na kila mtu alikuwa akimheshimu mama huyu. Nami nikawazia, “Vema, ataenda kwenye kijisanduku cha watu mashuhuri.”

262 Kwa hiyo, basi, nikasema, “Mara nyingine tena, wote walio upande *huu*, ‘Waleteni.’ Sasa upande *huu*, ‘Waleteni.’ Halafu wote walio katikati, sote pamoja sasa, ‘Waleteni watoto wadogo kwa Yesu.’”

263 Mara tu niliposema hivyo, mama huyu alikuwa tayari ameingia kwenye kijisanduku hicho. Ningeweza kuona, alipoingia kwenye kijisanduku hicho, kila mtu alisimama. Nao kwa namna fulani walikuwa wakifanya *hivi*, wakimtambua, naye alikuwa akiwatambua.

264 Nikawaza, “Vema, ni wakati wangu kuhubiri. Nitaenda nikawaombe wagonjwa.” Nikapanda *hapa* juu ya—juu ya mimbara, namna *hii*, nacho kile kijisanduku kilikuwa, loo, karibu tu kadiri alivyo ndugu huyu anayeketi *hapa*. Nikageuka, namna *hii*.

265 Nikawaza, “Vema, sasa, yule mama ataniinamia, kwa hiyo nitamtambua tu.” Na kwa hiyo wakati nilipogeuka, tayari alikuwa amekiinamisha kichwa chake chini, namna *hii*. Nilikuwa nikikiinamsha kichwa changu, namna *hii*. Ndipo nilipokiinua kichwa changu, wakati ule ule, nikutane naye, alikuwa ni mama, msichana, na mrembo.

Nikamwangalia. Nikasema, “Mama?”

Akasema, “Billy.”

266 Na papo hapo, radi ikaanza kumulika kote jengoni, ngurumo zikanguruma, nalo tetemeko likaja. Ndipo Sauti ikasema, “Usiogope juu ya mama yako.” Kasema, “Yeye yuko vile vile alivyokuwa katika mwaka wa 1906.”

Nami nikasema, “Ati nini, 1906?”

Ndipo Meda akasema, “Una shida gani?” Mke wangu.

Nikasema, “Mpenzi, 1906, 1906 ulikuwa ni nini?”

Akasema, “Kwa nini?”

Nikasema, “Ono, nimemwona mama amesimama papa hapa.”

Kasema, “Ati umeona nini?”

Nikasema, “Nimemwona mama.”

Akasema, “Hakika, Bill?”

267 Nikasema, “Naam. Alikuwa amesimama papa hapa, naye alikuwa ni mrembo. Na Yeye akasema . . .” Nikasema, “Alikuwa tu ni msichana mdogo.”

268 Kwa hiyo nikaenda nikachukua kumbukumbu ya kale ya familia. Mnajua alikuwa ni nani katika mwaka wa 1906? Bibi-arusi wa baba yangu. Huo ndio mwaka alipoolewa. Sasa yeye ni sehemu ya Bibi-arusi mwingine, Bibi-arusi wa Bwana Yesu.

269 Mtu fulani kutoka mahali fulani alinitumia nikeli. Ninayo hapa mfukoni mwangu, 1906.

270 “Naye Huyo, Roho Mtakatifu, atakapokuja, Yeye atawafunulia mambo haya ambayo nimeyasema, na atawaonyesha mambo yajayo.”

271 Sasa, ni kitu gani? Ile safari ya mawindoni ilikuwa tu ikiniandaa, mnaona. Moja ya safari nzuri kuliko zote nilizowahi kufanya, akijua hilo, mshtuko huu mkubwa. Huo ulikuwa ni upendo. Basi, ndugu, dada, kama maono haya mengine yote yamekuwa ya kweli kikamilifu, ya yale Roho Mtakatifu ameonyesha, haina budi kuwa ni Roho Mtakatifu. Biblia ilisema, ya kwamba, “Kama yakitimia, basi ilikuwa ni Yeye.”

272 Basi, ni tumaini jinsi gani tulilo nalo! Siku moja tutaondoka mahali hapa. Tutarudi tupate kuwa kijana mwanamume na mwanamke, tusione mauti tena. Afadhali nijue hilo kuliko kujua ya kwamba nitakuwa rais wa ulimwengu na niishi miaka milioni moja. Afadhali nijue ya kwamba nilikuwa mkononi mwa Mungu.

273 Nami nina furaha kujua, usiku wa leo, ya kwamba Yesu yeye yule aliyetoa tamshi hilo, Yeye yupo hapa, baada ya miaka elfu mbili. Mnaona, Hilo haliwezi kuangamia. Ni la Milele. Na ni Yesu yule yule usiku wa leo ambaye alikuwa siku ile aliyotoa tamshi hili. Na Yeye angali atalithibitisha Neno hilo, kama tutaliadini. Mnaamini hilo?

274 “Wakati Huyo, Roho Mtakatifu, amekuja, Yeye hatanena kwa shauri lake Mwenyewe. Lakini atayatwaa mambo, yaliyo Yangu,” hayo ni Neno, “na kuwaonyesha ninyi. Halafu, pia, atawaonyesha mambo yajayo.”

275 Katika Kitabu cha—cha Waebrania, mlango wa 4, Biblia ilisema, “Neno la Mungu lina ukali kuliko . . .”

276 Sasa, Neno alikuwa ni nani? Yesu. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Neno akafanyika mwili. Kukaa . . .”

277 “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wowote ukatao kuwili, ukichoma hata kugawanya, na kufikia mafuta yaliyomo ndani ya mfupa, tena Huyatambua mawazo ya moyo.”

278 Huyo ndiye Mungu wetu. Hatujapotea, enyi marafiki. Tungali katika neema ya Mungu. Na—najisikia, kuzungumzia chochote, na kuzungumza juu ya mambo yaliyopita . . . Na kama nilivyosema jana usiku, wakati hao wanafunzi walipokuwa wakijaribu kuuishia mkutano waliokuwa nao siku iliyotangulia, wakikutazamia mwingine, bali walisahau Muumba mwenyewe wa upepo na mawimbi alikuwa amelala kwenye hicho chombo.

279 Mungu aliyekuwa huko juu kwenye milima ile, kumweka dubu huyo mkubwa mkali mwenye ncha za fedha, kulingana na Neno Lake, anayelala pale sakafuni, kwa ajili ya ushuhuda.

280 Sasa, kama ukitaka kumwandikia mtu huyo, andika tu Bud Southwick, S-o-u-t-h-w-i-c-k, Bud Southwick, Fort Saint John, British Columbia, ndipo uache tu akujibie barua. Na jambo lingine, kama unaenda safari ya kuwinda, huyo hapo jamaa mzuri wa kuambatana naye.

281 Sasa angalia. Amesimulia hayo miongoni mwa wawindaji wote huku na huko kwenye barabara hiyo, mpaka ninaamini nitakuwa na mkutano mzuri sana wakati mwingine nitakapoenda kule, pamoja na viongozi tu, naam, kuyaona mambo hayo yakitukia jinsi tu yanavyotukia. Hiyo ilikuwa ni mwaka uliopita.

282 Hili ni mwaka huu, sasa hivi. Yesu yule yule aliyetoa ahadi hiyo, alisema, “Sitawaacha wala sitawapungukia. Nitakuwa pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Mnaamini hilo?

283 Pamoja na shuhuda kama hizo, pamoja na ukweli huo uliohibitishwa, ukweli halisi, tunawezaje kujisikia vinginevyo kuliko vile tu tungependa kupitia kwenye paa lile, tunyakuliwe? Hivi tumeviacha vitu vya ulimwengu kutuchosha akili, kwa njia kama hiyo, ambapo, tunaona mambo muhimu kama hayo ambayo ni ya hakika, yamethibitishwa kwamba ni kweli?

284 Sasa, kila mtu mgonjwa humu ndani, iwapo tu utamwamini yeye Huyo aliyeifanya ahadi hiyo, na kwa Yeye yule aliyeondoa kile kifafa kutoka kwa mvulana huyo, mtu huyo, Yeye ni

Mungu yule yule aliye papa hapa sasa. Kama ningaliwaondolea hilo, ningelifanya hivyo, bali siwezi. Yeye tayari ameyanunua hayo kwa ajili yenu, na jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuliadini.

²⁸⁵ Vipi kama mvulana huyo angalishikwa na kifafa, naye maskini mwanamke huyo aseme, “Sasa, hilo shati lina uhusiano gani?” Hilo labda lisingetenda kazi juu ya mtu mwingine yeyote. Mnaona? Ni yeye tu, maana limetumwa kwake. Naamani alijitumbukiza mtoni mara saba; lakini mtu mwingine, akijitumbukiza, labda wasingepona ukoma wao. Mnaona? Lakini angalieni. Yale asemayo ndiyo kweli, ukweli mkamilifu, uliothibitishwa.

²⁸⁶ Sasa, kunachelewa, kuita hata mstari wa maombi. Hebu—hebu tusimamishe hilo kwa dakika moja tu.

²⁸⁷ Hebu tuwazie tu. Hilo ndilo Mungu aliahidi? Huyu angekuwa ni Roho Mtakatifu halisi ambaye angefanya hivyo. Hiyo ni kweli? Vema, ni nani angeweza kusema ya kwamba Yeye hakuwa ni Roho Mtakatifu? Alikuwa hivyo. “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja.” Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Baba Yake. “Atazaa. Kitu hicho Kitakatifu kilichozaliwa ndani yake ni cha Roho Mtakatifu.” Kwa hiyo, Roho Mtakatifu na Mungu ni Roho yeye yule, na Huyu alikuwa ndani Yake.

²⁸⁸ Basi angalia yale aliyofanya wakati mwanamke alipoligusa vazi Lake, hapo alipolitazama kusanyiko hilo na kuyajua mawazo yao. Hivi Neno halisemi, ya kwamba, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Mpambanuzi wa mawazo ya moyo”? Hivi Yeye si anaahidi, katika Yohana Mtakatifu 12, ama Yohana Mtakatifu 14:12, ya kwamba, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya”? Ama, hivi limewahi kushindwa, ila kwamba ni kweli?

²⁸⁹ Basi, Mungu yupo hapa. Yeye yupo hapa kumponya kila mtu humu ndani. Yupo hapa kumwoko kila mtu aliyepotea. Na kabla sijafanya wito wa madhabahuni, kama ninavyojisikia kuongozwa kufanya, mnaona, kufanya wito huu wa madhabahuni, hebu na tumwite Yeye. Ni wangapi wenu watakaoacha, ama kusema, “Kama ninaweza . . .” Labda wageni hapa, waseme, “Sijawahi kuona mmoja wa mikutano hiyo. Ni—nimewasikia watu wakizungumza juu ya mambo haya, lakini kamwe si—sijawahi kuyaona. Lingenitia moyo kama ningeweza kuuona Uwepo wenyewe wa Kristo ukija miongoni mwa hawa watu na kufanya jambo lile lile alilofanya.” Lingewatia moyo?

²⁹⁰ Na tuinamishe vichwa vyetu; neno. Kila jicho lifungwe. Sasa hebu Roho huyo, anayelifuata Neno.

²⁹¹ Sasa, Baba, nimefanya, vizuri zaidi nijuavyo, Wewe unaujua moyo wangu. . . Tukijua ya kwamba watu hawa wanateseka chini ya joto hili, na kwamba wamesongamana ndani, wamesimama, bali wamekuwa na subira sana. Ninaweza

kuwazia lilikuwa ni kundi la namna hiyo lililosimama ufukoni siku ile na kukusikia Wewe ukinena kutoka kwenye kile chombo. Ndipo basi Wewe ukawaambia, “Tweka mpaka kilindini mkashushe wavu mvue samaki.” Sio ati muone kama kuna wengine mle. Walikuwa mle.

²⁹² Na jinsi hayo maneno muhimu ya mtume huyo aliyesema, “Bwana, tumevuta juya usiku kucha tusipate kitu; lakini hata hivyo, kwa Neno Lako tutashusha wavu.” Basi walipolitii Neno Lako, walishika samaki wengi mno, hata mpaka nyavu zao zikaanza kukatika.

²⁹³ Bwana Yesu, hapana shaka ya kwamba wanawake wengi waliachana na kufua kwao asubuhi hiyo, wanaume wengi wakaacha mashamba yao, kutoka kwenye mimea, wavuvi waliacha nyavu zao, wapate kulisikia Neno la Mungu. Bwana Yesu, kama ungalikuwa hapa katika umbo la mwili usiku wa leo, inatia shaka sana kama watu wengi zaidi ya waliokusanyika, wangekusanyika. Lakini watu hawa wanaamini ya kwamba Wewe hujafa, kwamba Wewe ulifufuka kutoka kwa wafu, na umelidhihirisha Neno Lako na kulitimiza Neno Lako, Neno ambalo nimewasomea kutoka kwenye Maandiko matakatifu usiku wa leo.

²⁹⁴ Na kama vile Bwana wetu wakati mmoja alipewa Biblia, ama Go—Gombo, naye akalisola, kisha akaketi chini. Na akasema, “Leo hii Maandiko haya yametimia.”

²⁹⁵ Jalia litukie tena, Bwana. Jalia liwe tena, kwamba siku ii hii, usiku uu huu, kwamba Maandiko ambayo nilisoma yapate kutimia. Nasi sote tumekuwa tukifundisha, kote katika juma, ya kwamba hilo lilipaswa kuwa ndilo jambo hasa litakalouthibitisha wakati wa mwisho. Ndipo basi mioyo yetu itaondoka, ikiwa na furaha.

²⁹⁶ Huenda kukawa na wengi hapa, Bwana, ambao unawazungumzia. Tusaidie usiku wa leo kulijua Neno Lako, Neno Lako lililothibitishwa kwamba ni Kweli. Tujalie, Baba.

²⁹⁷ Basi wakati vichwa vyetu vimeinamishwa, kwa ajili tu ya kukadiria, nipate kujituliza mwenyewe kutokana na kuhubiri. Ni wangapi wenu humu ndani, ambao kweli si Wakristo waliozaliwa mara ya pili? Sasa, huenda ukaenda kanisani, bali hilo silo ninalouliza. Wewe ni... Ikiwa wewe si Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, bali unaamini kuna Yesu aliye hai, Roho Mtakatifu halisi, nawe ungetaka kukumbukwa Kwake sasa, tafadhali, wakati kila kichwa kimeinamishwa sasa, nayo macho yamefumbwa, mwinulie tu mkono wako, “Bwana, nikumbuke”? Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni jambo zuri sana. Kunao wengine?

²⁹⁸ Sasa, sisi sio wengi sana kwa idadi. Lakini, hivi mnajua, ulimwengu ndio unaoangalia mambo makubwa na idadi kubwa?

Kama tulivyosema jana jioni, ilikuwa tu ile sauti ndogo, tulivu ndiyo iliyomvutia yule nabii ajitokeze huku uso wake umetiwa utaji.

²⁹⁹ Sasa, wewe mwamini Mungu. Ndugu yangu, dada yangu, mwamini Mungu. Basi iwapo Bwana wetu Yesu mkuu, mwenye fadhili atakuja ambapo Neno hili limewekwa hapa, Neno Lake Mwenyewe, limefunguliwa, na kuwathibitishia ya kwamba huyu Roho Mtakatifu, ninayenena habari Zake, ni wa Kweli! Huenda ulichanganyikiwa mara nyingi na mambo mengi, lakini hilo linaonyesha tu ya kwamba kuna lililo Halisi mahali fulani. Basi wakati Yeye anapofanya hilo, ninawatakeni ninyi mlio inua mikono yenu juu, mje, mnione, kwa muda mfupi tu.

Sasa mwaweza kuinua vichwa vyenu.

³⁰⁰ Bwana Yesu, ichukue ibada hii mikononi Mwako sasa. Mimi ni mtumishi Wako. Na mahubiri yote... Neno moja tu kutoka Kwako litamaanisha mengi zaidi kuliko yote ambayo tungeweza kusema maishani; Neno moja tu. Lijalie sasa, Baba, ninapoukabidhi huu, shuhuda hizo. Unajua kwamba ni za kweli, Baba. Wewe Ndiwe uliyezitoa. Na kamwe hazijawahi kushindwa. Tujalie, katika Jina la Yesu. Amina.

³⁰¹ Sasa, ni watu wangapi hapa ndani, ambao hawana kadi za maombi, walio wagonjwa? Inueni mikono yenu, kila mahali jengoni, wasio na kadi za maombi, na ni wagonjwa. Vema. Na wale walio na kadi za maombi, inua mkono wako. Ni karibu sawa. Nazo zote zimechanganyikana.

³⁰² Sasa, kulitazama kusanyiko, kwanza, kuwa mwaminifu mbele za Mungu na mbele za... zenu. Ninajua ya kwamba, ninaangalia *hapa*, kwamba baadhi ya rafiki zangu wameketi kwenye kona *hii* hapa. Ndugu Noel, nanii wa—wake... na Dada Jones, na Ndugu Outlaw, mwanangu, ndugu hawa *hapa*, na Ndugu Moore. Simjui ndugu *huyu*, bali nimemwona katika mikutano, mara chache za mwisho. Siwezi kulikumbuka jina la ndugu *huyu*, pia, bali ninamjua tu kwa uso. Dada papa *hapa*, Dada Williams. Dada Sharrit aliyeketi pale pembeni. Huko nyuma kabisa kuna watu kutoka kwenye maskani huko Jeffersonville.

³⁰³ Anayeketi papa hapa ni rafiki yangu wa thamani wa zamani, mwenye umri wa miaka tisini, anayetoka Ohio, anaendesha motokaa kuvuka nchi. Nami ninaondoka kwenda Afrika, naye pamoja na mke wake mpendwa waliniomba kama wangeweza kwenda Afrika pamoja nami. Kasema, “Tutaomba...” Umri wa miaka tisini, ndugu Mjerumani, kamwe hakumjua Bwana. Wakati nilipohubiri usiku mmoja, yeye aliingia amevaa nguo zake nzuri, akabatizwe. Umri wa miaka tisini! Nje ya...

³⁰⁴ Ninaamini, loo, huyu ni Ndugu Waldrop na Dada Waldrop wameketi *pale*. Sasa, hao karibu ndio umbali... na Ndugu Borders. Sasa, karibu ni hao.

305 Sasa, ninayaita majina yao. Sasa, kama ninyi mnaonijua jinsi hiyo, msiombe. Mnaona? Niombeeni. Mnaona?

306 Lakini ninawatakeni ninyi msionijua mimi, nanyi mnajua ya kwamba siwajui, ninawatakeni msemi moyoni mwenu, “Bwana Yesu, nimeyasikia haya yakinenwa. Ni—nimemsikia mhudumu huyu usiku wa leo akisoma hili kutoka kwenye Biblia. Nilisikia shuhuda hizo, nami nimesikia kama hizo, mwajua, za nyakati mbalimbali hili lilipotendeka. Hivi tumeukaribia mwisho hivi, Bwana? Tumeukaribia hivi?”

307 Kumbukeni, wakati ishara hiyo ilipofanyiwa sodoma, ule mji ulioteketezwa, Yesu aliurejea, kasema, “Kama ilivyokuwa...” Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho waliyopokea kabla huo mji haujaangamizwa. Naye Yesu alisema ya kwamba hilo litarudiwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.

308 Sasa, mnajua hiyo ni kweli, jinsi ambavyo... Mungu, Mungu katika mwili! Ni wangapi wanaoamini huyo aliyenena na Ibrahimu alikuwa ni Mungu? Naam. Vema, Biblia inasema, “Elohimu,” kwa hiyo, huyo—huyo ni yu—yu—yule Muumba wa mbingu na nchi, Yeye ajitoshelezaye kwa yote. Alikuwa ndiye.

309 Alikuwa akionyesha nini? Alikuwa katika mwili wa mwanadamu, akasimama pale na kula nyama ya ndama, na kunywa maziwa kutoka kwa ng’ombe, na kisha angeweza kutoweka asionekane kwa macho. “Nitakurudia kulingana na wakati niliokuahidi.” Mnaona? Akamwita kwa jina lake. Na huku ameugeza mgongo Wake, kasema, “Yu wapi Sara?”

Kasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

Kasema, “Nitakurudia kulingana na wakati wa uhai.”

310 Naye Sara kasema, “Humm, humm,” nyuma hemani.

311 Akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Kumbukeni, Biblia ilisema alikuwa hemani nyuma Yake. Kasema, “Kwa nini Sara akacheka?”

Sara akasema, “Sikucheka.”

Akasema, “Ndiyo, ulicheka.” Mnaona? Hiyo ni kweli.

312 Mtu amesimama pale, Mungu akijiwakilisha Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu. Yesu alisema ingekuwa vivyo hivyo katika kuja kwa Mwana wa Adamu: Mungu katika Kanisa Lake, wewe, mimi, akijiwakilisha Mwenyewe. Sasa, kulikuwako na maskini mwanamke mmoja...

313 Wakati Mungu alipokuwa ndani ya Kristo, Yeye alikuwa na Roho kwa ukamilifu. Yeye alikuwa Mungu. Mimi ni mmoja tu wa watumishi Wake, na wewe ni mmoja tu wa watumishi Wake. Tunaye Ro—Roho kwa—kwa kipimo. Yeye alikuwa Naye bila kipimo. “Ndani Yake mlikaa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili.” Ndani yangu ni karama ndogo tu, na ndani yako mna karama, Yake. Lakini, haidhuru ni ndogo vipi, ni Roho yule yule.

314 Sasa, kama huyo ni Roho wa Mungu, atafanya kazi za Mungu. Sasa, wewe omba na useme, “Bwana Yesu, maskini mwanamke mmoja wakati mmoja aliligusa vazi Lake.” Nasi tunasema. . .

315 Huku katika Agano Jipya, alisema katika Waebrania, alisema, “Yeye ni Kuhani Mkuu sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Ni wangapi wanaojua hiyo ni Biblia? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Vema, hilo halina budi kuwa ni kweli.

316 Vema, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, angekujibu namna gani? Kama vile Yeye alivyofanya jana, kama Yeye ni yule yule leo.

317 Sasa, wewe omba na kusema, “Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako. Halafu basi, Wewe umempa Ndugu Branham karama ndogo, kututia moyo. Na yeye haniujui. (Nimeketi *huku* nyuma sana; na *huku*; na *hapa* chini; na popote ambapo nimeketi. . .) Yeye haniujui mimi, bali Wewe unanijua. Basi jalia nimwone Roho Wako mkuu, Bwana. Sio kuwa inanibidi kulifanya, lakini ni kusaidia tu kunitia moyo na hao wengine, kwa sababu tumelisoma Neno. Jalia niguse vazi Lako, kisha Wewe unijibu moja kwa moja. Jalia nitumiwe usiku wa leo, Bwana, kwa kusudi hilo. Itaonyesha kusanyiko lote kwamba Wewe ungali hai.” Hilo lingekuwa ni la ajabu kama Yeye angefanya hilo?

318 Sasa, wewe kwa namna fulani omba tu, wewe mwenyewe, kwa utulivu. Useme, “Bwana, jalia niguse vazi Lako.” Nami nitajitolea kwa Roho, halafu basi Roho Mtakatifu na afanye yaliyosalia. Maana, sasa, nimezungumza, nikashuhudia, bali siwezi kufanya zaidi sasa. Nimefika mwisho wa safari yangu.

319 Ninaliangalia tu kusanyiko, kuona kama mimi. . . Sina budi kuliona, mwajua. Mnaelewa hilo.

320 Nyuma mkono wangu wa kushoto, huko nyuma kabisa, yapata katikati nyuma ya hili jengo, yupo mwanamke anayeomba. Yeye yuko karibu kufa, Mungu asipomsaidia. Ana kansa, nayo hiyo kansa iko kwenye titi lake. Loo, naomba asiukose!

Nisaidie, Ee Bwana.

Dada, kama utaamini! Loo, jamani! Ataikosa.

Bwana Yesu, tusaidie, tunaomba.

321 Mary May. Haya basi. Hivi hatufahamiani mmoja kwa mwingine? Sikujui. Hunijui mimi. Huo ndio uliokuwa ugonjwa, na kile. . . kila kitu kilichosemwa kilikuwa ni kweli? Basi, amini. Utakwisha. Amina.

322 Sasa, kutoka kwenye giza lililokuwa juu yake, ni nuru. Hakika tu kama yule mvulana, kile kifafa kilivyomwacha. Mungu yeye yule, Yule aliyekuwa huko juu katika misitu ya

kaskazini, ndiye Mungu yeye yule hapa. Endelee ni tu kuamini. Amina. “Kama unaweza kuamini!”

³²³ Hii hapa juu ya mwanamke anayeketi hapa mbele yangu. Ana kasoro mgongoni mwake. Ni ggedu, mgongoni mwake. Yeye—yeye hatoki hapa. Ametoka Montana. Jina lake ni Binti Stubbs. Simama, poka uponyaji wako katika Jina la Yesu Kristo.

Haikubidi kusukuma. Tulia.

³²⁴ Jamaa mkubwa anayeketi hapa, akiniangalia, akifanya *hivyo*. Amini. Utapata afya. Una ugonjwa wa wasiwasi. Kama unaamini, Mungu atakuponya.

³²⁵ Mama huyo aliye na ugonjwa wa kike. Amini, nawe unaweza kupata afya. Rudi nyumbani, na umwamini Mungu. Ni kwa nini nilisema urudi nyumbani? Itakubidi kurudi New Mexico, kufika kule, Bw. na Bibi Watkins. Sasa, unajua mimi sikujui. Amina.

³²⁶ Mama huyo aliye papo hapo nyuma yako, aliye na kidonda hicho mguuni, Binti Brown. Utaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unaonekana kuvutiwa sana. Sasa, unajua sijawahi kukuona maishani mwangu. Kwenye mguu wa kushoto. Sasa, wewe amini kwa moyo wako wote, utakuwa mzima.

³²⁷ Mama anayejaribu kusogea, naye yuna baridi yabisi. Inamfunga, vibaya. Bibi Fairhead, amini kwa moyo wako wote, nawe utapata afya. Sasa, unajua sijawahi kukuona maishani mwangu. Huyu, loo...[Dada huyo anasema, "...ponywa hapo awali. Nimeponywa hapo awali, nami ninajua Hiyo itaniponya."—Mh.] Amina. Naam.

³²⁸ Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Sasa, Yeye atafanya nini? “Yeye atayachukua mambo ambayo nimewaambia, na atawaonyesha. Halafu basi Yeye atawaonyesha mambo yajayo.” Mnaona ninalomaanisha? Mnamwamini?

Sasa hebu tuinamisha vichwa vyetu tena.

³²⁹ Sasa, wewe unayejua ya kwamba kama ungeyaaga maisha haya usiku wa leo, kwamba ungekuwa...usingekuwa...ungekuwa umeondoka, hujazaliwa mara ya pili. “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona ule Ufalme.” Mbona usije papa *hapa*? Simama hapa tukuombe, papa hapa, kwa dakika moja. Utakuja sasa hivi katika Uwepo wa Roho huyu?

³³⁰ Hamtaona kamwe kitu chochote kikitukia kilicho kikuu zaidi mpaka mtakapokuona kule Kuja kwa Bwana. Sasa, kumbukeni tu. Hakika ninajua lile ninalozungumzia, la sivyo Yeye asingejalilia hii huduma. Usiliache likupite sasa. Hivi wewe ni mwaminifu?

³³¹ Waweza kuja? Usipokuja, basi, kati yako na Mungu, ndipo limekaa. Mimi sina hatia. Niko huru na damu yote, kwa sababu nimewaambia Ukweli. Nimewahubiria Neno. Nimewaambia

kile Yeye alichokuwa. Na Yeye, wakati alipokuja, Yeye alithibitisha kile alichokuwa wakati huo; na Yeye ananijalia kuthibitisha kile Yeye alichosasa. Yeye ni sawa na alivyokuwa wakati huo. Mnaamini jambo hilo?

³³² Basi, ni wagonjwa wangapi walio humu ndani basi, wengine walio hapa ambao ni wagonjwa? Inueni mikono yenu.

³³³ Sasa wekeni mikono mmoja juu ya mwingine, na hebu tuombe maombi ya imani kwa ajili yenu.

³³⁴ Sasa ninataka kuwaulizeni jambo fulani, kwa utulivu. Kama Mungu, kama Mungu anaweza kuja na kufanya mwujiza huo! Muujiza ni kitu ambacho hakiwezi kuelezeka. Sasa, kama ukitaka kumhoji yeyote wa watu hawa huku, nenda kawahoji, wakati wowote mahali popote. Unaona? Kumbukeni tu, ni Mungu. Haya hapa ni maono tu ya kawaida. Nani—nani, ni kitu gani kinachofanya hivyo? Ni wewe, mwenyewe. Ninyi ndio mnaoyafanya hayo.

³³⁵ Unaona, wakati yule mwanamke alipoligusa vazi Lake, Yeye alisema, “Nguvu zimenitoka.” Lakini wakati Baba alipomwonyesha habari za Lazaro, na Yeye akaondoka kisha akarudi, na kumfufua Lazaro katika wafu, kamwe Yeye hakusema, “nguvu.” Huyu alikuwa ni Mungu akiitumia karama Yake Mwenyewe, na hiyo wengine ilikuwa ni mwanamke akiitumia karama ya Mungu.

³³⁶ Mimi si karama ya Mungu. Yesu Kristo ndiye Karama ya Mungu. Ni karama tu aliyonipa Yeye, kwamba nilizaliwa namna hiyo, huku dhamira ya ndani na dhamira (dhamira ya kwanza) zikiwa papo hapo pamoja. Hulali; unaliona tu. Roho Mtakatifu anakuja juu ya dhamira ya ndani kama tu anavyokuja juu ya dhamira ya kwanza. Kama akija katika dhamira yako ya ndani, utakuwa na ndoto ya kiroho. Akija juu ya yangu, mimi sioti. Ninaangalia pale tu na kuliona. Mnaona? Basi, tunazaliwa, huwezi kujifanya kitu chochote tofauti. Umezaliwa hivyo. Unaona? “Karama na miito havina majuto.” Ni za kufanya nini? Kumdhihirisha Yesu Kristo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

³³⁷ Huku mikono yenu imewekwa mmoja juu ya mwingine, ninatumaini ya kwamba utaiweka roho yako katika uangalizi wa Mungu sasa hivi, “Bwana, nichunguze. Hivi nimetiwa ganzi sana na mambo ya ulimwengu, hata ninashindwa kuona saa hii kuu inayopita?”

³³⁸ Mnajua, hivyo ndivyo imekuwa daima. Ilipitia moja kwa moja kanisani, wala hawakujua. Hiyo ni historia. Msiache ipite, marafiki, kuona neno likithibitishwa, tena na tena, kuliona Neno la Mungu likidhihirishwa, na ule Utu wenyewe wa Yesu Kristo unaingia moja kwa moja miongoni mwa watu hawa na kufanya jinsi hasa Yeye alivyofanya hapo awali.

³³⁹ Baba wa Mbinguni, ninajisikia sasa, Bwana, ya kwamba Neno Lako lilisomwa. Ushuhuda ulitolewa. Roho Mtakatifu alishuka na kulithibitisha Neno hilo pamoja na huo ushuhuda. Sasa liko mikononi mwa watu, Bwana. Liko pajani mwao. Hakuna kitu kingine ninachojua kusema. Wala sijui jambo lingine lolote uliloandika katika Neno, ambalo Wewe ungefanya, kwa kuwa tayari umewaponya. Ni kuwafanya tu waliamini. Na Wewe kufanya jambo kama hili, nasi tungewezaje kulitilia shaka tena? Tungewezaje kumruhusu Shetani kutia ganzi dhamira yetu muda mwingine tena?

³⁴⁰ Shetani, ninatangaza uponyaji huu juu ya watu hawa, na kukwambia, “Nakuapisha, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, toka hapa. Toka, katika Jina la Yesu Kristo, na uwaachilie watu hawa waende.”

³⁴¹ Sasa, kama unamwamini Yeye, simama kwa miguu yako. Unaamini? Simameni kwa miguu yenu basi, mkampe Mungu sifa. Simameni mkaamini. Msilitilie shaka tena.

³⁴² Katika Jina la Yesu Kristo, jalia Roho Mtakatifu alete furaha, nguvu, ufufuo, Uzima kwa watu hawa, Bwana.

³⁴³ Mpeni sifa sasa, na mlibariki Jina Lake takatifu. Tunampenda. Tunamsifu. Tunamsujudu, Yeye asiye na kifani, Yule wa Milele, Mwana wa Mungu aliye hai. Katika Jina Lake, mpokeeni. Yeye yupo hapa. Amina.



ROHO WA KWELI SWA63-0118
(Spirit Of Truth)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Ijumaa jioni, tarehe 18 Januari, 1963, katika Kanisa la Mataifa Yote huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyoerekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org